# *Kama Mungu Yu Pamoja Nasi, Basi Yako Wapi Matendo Yake Ya Ajabu?*

Asante, Ndugu Neville, na habari za jioni, marafiki. Nimerudi tena. Sikupata ila masaa manne asubuhi ya leo. Hiyo ni aibu. Na baada ya kuzungumza kwa masaa marine, mnapaswa kuwa mmechoshwa sana nami, mngenifukuza jukwaaani.

2 [Kusanyiko linasema, "La!" Nduguye Ndugu Branham, Doc, anasema, "Hilo linanikumbusha. Lakini mtu fulani alisema leo kwamba siku zote una chungu nzima ya mambo haya yaliyosalia, ambayo huwahi kamwe kuyazungumzia."—Mh.] Ndiyo, bwana. ["Lakini jioni ya leo, Mpenzi, waweza tu kuchukua muda wote unaotaka." Kusanyiko linasema, "Amina!" Doc anasema, "Kwa hio, haikubidi kuacha lo lote."] Nina kama nusu ya Biblia imeandikwa hapa. [Mtu fulani anasema, "Unao siku mzima, wa kuhubiria."] Tunao ndugu wengi wa thamani hapa, twataka kuwasikiliza.

3 Wangapi walifurahia ibada asubuhi hii, ile. . .[Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, masaa manne. Sijui kanda ile ilichukua muda gani.

4 Dada yangu alinipigia simu, baada ya ibada, naye alisema, "Haikupaswa iwe kwa mtu mwingine." Kasema, "Lazima ilikuwa kwa ajili yangu tu. Nami nikasema," kwa mumewe, "'Junior,' nikasema, 'ungesemaje?' 'Loo', akasema, 'Nimemsikia Ndugu Branham akifanya vyema zaidi ya hivyo.'" Akasema, "Basi nilikuwa na hakika yote yalinijia mimi," akasema.

5 Naamini yuko nyuma kule, la sivyo, ningemsengenya, lakini nitaliachilia tu. Delores, uko wapi? Hayupo hapa. Vema, nitalisema basi. Alisema, "Nimekuwa na hatia ya kutumia, wajua, vipodozi vidogo; kukata kidogo tu." Kasema, "Hiyo imekwisha." Alitambua alikuwa hajakufa bado, unaona. Yakubidi ufe, hivyo niliuita ujumbe wa. . .wa Mwaka Mpya. Bwana na atujalie baraka Zake.

6 Vizuri sana, usiku wa leo, kuona wengi sana wamo ndani. Ndugu Graham Snelling, niliingia tu kwa wakati kumsikia akiumalizia wimbo ule wa zamani, "Nasi Tutaenda Kukaa Katika Mlima Wa Sayuni."

7 Nadhani hakuna mtu hapa anayemkumbuka maskini Rabbi Lawson. Kuna mtu ye yote anayemkumbuka? Ndiyo, wawili

au watatu wenu, Ndugu Graham na Ndugu Slaughter. Hilo lilinifanya nimfikirie Ndugu Lawson. Mwakumbuka jinsi ambavyo alikuwa akiimba? Jamaa, mdogo, nilimuita “rabbi” kwa sababu alivaa kofia ndogo, nyeusi, yenye mabapa. Alikuwa mhubiri wa Kipentekoste. Lakini, miwani mikubwa ya gamba la kasa, na nilisema, “Unaonekana tu kama rabbi.” Na kwa hiyo sikuzote tulimwita, “Rabbi Lawson,” ndugu mzuri mdogo. Naye yeye a—alikuwa mzee sana, aliingia ameinama; alikanyagwa na gari, na magoti yake yakakakamaa. Angetundika mkongojo wake, au bakora yake, upande *huu* hapa. Nami ningeketi chini kwenye kiti. Na alipofika pale kwenye sehemu ile, “Gurudumu zote za uhai usiodumu zitasimama kimya,” angeokota hiyo bakora ya kale, akapitisha mkono wake begani mwake, na kuipachika shingoni mwangu na kunivuta moja kwa moja, namna *hii*, akanikumbatia, na kusema, “kisha *sisi* tutaenda kuishi katika mlima wa Sayuni.”

8 Ye yote, kuna mtu mwingine hapa aliyewahi kumjua Rabbi Lawson? Wachache wenu tu. Nataka kusema hili, basi. Kitu cha ajabu kilitukia kwake. Alikuwa mhubiri halisi na mdogo, ndugu mzuri. Na yeye—yeye hakuwa na huduma kubwa; huo haukuwa mwito wake. Lakini naamini aliishi mwaminifu kwa agizo lake, hicho ndicho kitu muhimu.

9 Na mkewe alifikiria hapati fedha za kutosha, akihubiri, kwa hiyo alimtaka apate kazi. Alijifunza Biblia wakati wote. Kwa hiyo siku moja alimkasirikia sana, akainyakua Biblia toka pajani mwake, akaichukua, akaifungua stova, kisha akaitupa katika stova akaichoma moto. Miezi michache baadaye, alikuwa anawasha taa za Krismasi, ule moto wa mti wa Krismasi ukamshika na ukamteketeza, mahali pale pale. Unaona, unavuna unachopanda. “Msiguse masihi Wangu, wala msiwadhuru manabii Wangu.” Unaona?

10 Tukifikiria kuhusu Neno la Mungu. Hao watu ambao walipata ajali kule, kisha Shetani alijaribu kuharibu. . .Ndio tu nawaona wakiinuka nyuma kule, papo hapo, kuruhusu mtu fulani aingie. Trela yao, karibu kila kitu katika chumba kile kiliungua kabisa. Nilikuweko huko. Kitu tu kilichonusurika, nafikiri, ni Biblia ya kale ililobarikiwa na, nafikiri, kitabu changu na cha Ndugu Osborn. Kila kitu kiliungua kikawa majivu, katika trela yao. Nikaiokota ile Biblia, ilipata moshi kidogo tu nje. Nilimwambia yule dada na ndugu kwamba siku moja, Bwana akipenda, ningependa kuileta hiyo mimbarani hapa, na kuhubiri juu ya kifungu, “Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita.” Wakati kila kitu kimekwisha, Neno bado lipo hapo. Je! si inastaajabisha jinsi Mungu anavyotunza Neno Lake? Basi hebu Neno hilo liwe ndani yako, Yeye atakutunza. Hiyo ni kweli.

11 Wakati wa yale mafuriko. Nilikuwa ninahubiri hapa usiku mmoja, nikaacha Biblia yangu. Mafuriko ya ’37 yalikuja katika

karibu usiku mmoja, yalipovamia Maskani; yakainua mimbara hii hii, yakaiinua moja kwa moja juu (hapakuwa na dari nyingine hapa ndani wakati huo) na yakaiegemeza moja kwa moja kwenye dari. Neno likiwa chini ya mimbara; badala ya kuzama, lilielea, yakaliinua hadi kwenye dari. Na nilipiga makasia mahali pote hapa, katika mashua. Na kisha wakati maji yalipopungua, ilishuka na ilikuwa imekaa papa hapa kwenye sura ile ile niliyokuwa nikisoma, baada ya mafuriko. "Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita." Hiyo ni kweli. Yeye ni wa ajabu. Sivyo?

12 Kwa kweli, na—nataka kuondoka hapa, upesi sana, kwa sababu wana wahudumu wengi wazuri sana. Nilifikiria ningewaita wote jukwaani, lakini hatuna viti kwa ajili yao. Kwa sababu, nimeona wengi tangu nilipokuja hapa, katika kusanyiko, labda wana ujumbe usiku wa leo. Twataka kusikia kutoka kwa mchungaji wetu, toka kwa watu mbalimbali, u—ujumbe walio nao mioyoni mwao, kwa usiku wa leo. Nami nitanena kwa kifupi sana, na kujaribu kusema kitu kidogo.

13 Na basi tunaanza jambo fulani usiku wa leo, au kitu fulani kinachotendeka usiku wa leo, kama Mungu akipenda, ambacho hatujawahi kutenda tangu nime . . . maishani mwangu. Nililifikiria tu hilo hivi majuzi, nikamwita Ndugu Neville, naye alifikiria ni wazo zuri sana. Badala ya vurugu zote za kupiga filimbi, na kupiga vifijo, na kutenda mambo yasiyofaa, na kunywa pombe, na karamu za ulevi wa Mwaka Mpya, na mambo kama hayo, tutakuja madhabahuni na kushiriki meza ya Bwana, usiku wa manane. Na . . . Na kila mmoja wetu, tunaposikiliza maneno usiku wa leo, toka kwa wahudumu hawa mbalimbali, hebu na tuwe na kicho sana.

14 Sasa usiku wa Jumapili iliyopita, nilitoa Ujumbe wa Krismasi. Na kisha nikazungumza na Kanisa, na watu toka Georgia na sehemu mbalimbali, "Msije," sababu ingewaondoa watoto wao kwenye Krismasi. Wana . . . Wanaitazamia, wao ni watoto tu. Na ningewapelekeeni kanda. Sasa, ninyi ambao hamkupata kuja, nitaigharimia ka—kanda. Wajulishe tu Ndugu Woods na wengine, na nita—nitalishughulikia jambo hilo kwa ajili yenu, na kuipata kanda.

15 Na sasa, usiku wa leo, nataka tu kwanza kusema jambo hili moja, kabla ya kusoma somo langu.

16 Na labda, katika kuhubiri, tutaendelea hadi, karibu usiku wa manane. Na kisha sisi, yapata dakika kumi na tano, ishirini, kabla ya saa sita, tunatoka na kuleta mkate wa kosha, Me—Meza ya Bwana, mwana kondoo wa pasaka. Na kuuweka hapa, mkate, na kisha kutoa shukurani kwa Mungu, na kusimama madhabahuni, vichwa na mioyo vimeinamishwa, na kushiriki Meza ya Bwana. Nami nafikiri chumba kimejaa vinasasauti mle ndani, na kadhalika. Sijui kama tuna . . . Wasemaje? Watakuwa

wameisha toka wakati huo, kwa hiyo haitatulazimu kuacha kutawadhana miguu, pia. Na kesho ni Jumatatu na baadhi ya watu, wanaotoka nje ya mjini, wanao muda wa kutosha kwenda nyumbani. Na nikitumaini kwamba Mungu atawabariki sasa.

17 Na huu utakuwa labda wakati wa mwisho nitakaokuwa nanyi, hadi nitakaporudi kutoka Magharibi. Naenda Arizona, labda nikienda Louisiana kwanza, kisha niendelee hadi Arizona na California. Na basi mara tu nirejeapo, natumaini kuwa nanyi tena. Hadi wakati huo, ombeni.

18 Sikujipangia utaratibu wa safari. Naamini ninamuona Ndugu Borders, usiku wa leo, mkutanoni. Nilimwashiria asubuhi hii. Na yeye huweka ratiba, naye alinipa kitabu hivi majuzi, cha kila aina ya makaribisho. Lakini kwa namna fulani, wakati huu, Roho Mtakatifu aliniambia, "Enenda mahali pamoja. Na ukimaliza hapo, nitakuambia utakwenda wapi kutoka huko." Unaona, huongoza tu moja kwa moja hivyo, la kutenda baadaye. Kwa hiyo yatubidi tuwe waaminifu sana, wakati Yeye aanzapo kufanya hivyo, unaona, ujue tu po pote mtu anaita na kungojea.

19 Si kwa azimio la Mwaka Mpya, sababu hatufanyi hayo; hayana faida, unayavunja. Nimemuona baba yangu akitupilia mbali lile bumba la tumbako kila usiku wa Mwaka Mpya; anaangalia alipolitupa, ili aweze kulichukua kesho yake. Unaona? Na hivyo ndivyo kadiri mambo yanavyokwenda. Hebu tusifanye maazimio. Na tuombe rehema na neema, tuombe rehema ya Mungu.

20 Na kama sipati nafasi tena, ya kuja kuhudumu Meza ya Bwana, labda katika kuharakisha wakati huo, mimi... Hili ndilo jambo moja ninalotaka kufanya; moja ya shauku zangu ni kuona Kanisa bila ya ila wala kunyanzi, ambalo Roho Mtakatifu...Ndugu Grim, hii imekuwa shauku ya moyo wangu; kuona Kanisa ambalo limejawa sana na Mungu, mpaka dhambi haiwezi kukaa ndani yake po pote, Roho ya Mungu ikiipambanua, po pote ilipo. Nataka kuona hilo.

21 Na jambo moja ambalo ninatamani, ono moja kubwa kutoka kwa Bwana ambalo siku zote nimetamani kutoka kwa Bwana. Alinipa hilo hivi majuzi asubuhi, mnamo saa nne asubuhi. Na hilo liliridhisha shauku yangu. Kwa miaka na miaka, tangu nimekuwa mhudumu, nimetamani kuona hilo, na hatimaye likatimia. Sasa ninamshukuru sana Mungu. Sikusema cho chote kuhusu hilo, nimeliandika tu. Nami najua ni sawasawa tu na jambo ambalo nimekuwa nikiomba, wakati wote.

22 Na sasa naomba na kumtumainia Mungu. Na usiku wa leo, upya, najitoa maisha yangu Kwake Yeye, juu ya mimbara Yake. Shauku hiyo moja kubwa katika maisha yangu ni kuwa mnyenyekevu zaidi mbele za Mungu na mbele za watu Wake. Nikijua kwamba hilo ni moja ya makosa yangu makubwa,

ni kushughulika na watu hivi kwamba, imeondoa mambo mengi kwangu, ambayo nilikuwa nayo. Natumaini kwamba Mungu atarejesha tena ile furaha ambayo nilikuwa nayo wakati mmoja. Si kwamba ati nimepoteza furaha yangu, la; lakini ninamaanisha nahitaji mwingi zaidi, unyenyekevu mwingi, mwingi zaidi, kumtumikia Bwana. Mwaka huu ujao, nimemuahidi Mungu, kama ataniacha niishi, na kunipa afya na nguvu, nitajaribu kuwa mtumishi kwa Mungu, na ndugu kwa wanadamu, kwa moyo wangu wote.

Mungu awabariki sasa. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mdogo.

23 Wakati ulimwengu, Baba, unapopepesuka kwenye ikweta, kama tunavyoambiwa, sasa utaanza tena kurudi nyuma kuelekea . . . toka siku fupi sana ya mwaka, hata iliyo ndefu sana. Muda mfupi tu, na filimbi zitapigwa, watu watapiga makelele, kengele zitalia; na mwaka wa zamani umekwisha, na mwaka mpya unakuja. Baba, tunakushuru, kwamba, Wewe umeturuhusu kuuona mwaka huu wa 1961. Na tunaomba utusamehe dhambi zetu zote ambazo tumetenda katika mwaka huu. Na kama kumekuwa na kitu kimoja ambacho tumetenda ambacho kimekuwa chema, Jina Lako na lisifiwe. Kwani haikuwa sisi, tusiostahili; lakini ilikuwa Wewe, Roho Mtakatifu ambaye hatimaye alijiingiza katika maisha yetu, juu ya hali zetu za uasi, na kufanya jambo lililomtukuza Mungu. Tunashukuru kwamba Yeye alifanya hivyo. Baba, tungeomba usiku wa leo kwamba Yeye angetusukuma kando kila wakati, na kuacha mapenzi ya Mungu yafanyike katika maisha yetu.

24 Na usiku wa leo, wakati makanisa tunayoshiriki nayo, wachungaji wao wanaketi hapa; Ndugu yetu Graham, na ndugu toka sehemu mbalimbali nchini; Utica, Sellersburg, na Georgetown, po pote pale. Watu wa thamani wamekusanyika pamoja, toka nyingi, hata mikoani, usiku wa leo, kutusaidia sisi katika sikukuu hii kubwa ambayo tunaiadhimisha; na wamefanya wakati huu kuwa wa kuimba nyimbo, kuomba dua, na wa kusikiliza Neno la Mungu. Jaza kila moyo. Ondoa kila shaka. Ondoa kila hofu. Ondoa uchovu wote. Na mruhusu Roho Mtakatifu aingie mioyoni mwetu, na kulipanda Neno. Na tuwe shamba ambamo Neno litaangukia, ambamo litazaa matunda mwaka ujao. Tujalie, Bwana.

25 Nisaidie sasa, kwani ni wakati wangu, kura imeniangukia wakati huu, kuzungumza. Naomba kwamba utayapaka mafuta maneno yanayosemwa. Na yatoke chini ya upako wa Roho Mtakatifu, kwa matazamio, Bwana, kuwaleta watu, ambao hawakujui Wewe, Kwako; na wale walioko, na wawe na imani zaidi, kukutumikia Wewe. Tujalie, Bwana. Na isaidie sauti yangu, kwa kuwa nina mafua mabaya na nimechoka kwa kutoa Ujumbe wa masaa manne asubuhi hii, naomba kwamba Wewe

utanisaidia. Tusaidie sisi sote, na ututayarishe sasa kwa ajili ya ibada ijayo na ushirika.

26 Bariki kanisa hili na mchungaji wake, Ndugu yetu Neville, wadhamini wake na mashemasi wake, na watumike kwa ushujaa zaidi mwaka huu kuliko wakati wo wote uliopita. Asante kwa kazi yao na ushujaa wao. Jinsi walivyoniunga mkono nilipohitaji mtu wa kuniunga mkono! Ndugu Neville na Ndugu Roy Roberson, na ndugu wote wa thamani walioshikamana nasi katika nyakati za shida, na, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, walikata kauli vizuri sana jinsi walivyojua. Na kauli walizokata, zimehakikishwa kuwa katika mapenzi Yako, kwani Wewe umebariki kauli zao. Mungu, endelea kuwa pamoja nao. Tusaidie sisi sote, pamoja sasa. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

27 Sasa, kwenu ninyi mnaoandika vifungu; na nikiamini kwamba mtakuwa mnaniombea. Na kwa muda mfupi, ningependa kuwaelekeza kwenye kisehemu cha Andiko kipatikanacho katika Kitabu cha Waamuzi, kwenye sura ya 6, kuanzia aya ya 7. Naomba kwamba mngesikiliza kwa utulivu, na msikilize Neno.

28 Mwaweza kunisikia huko nyuma, sawa? Inueni mikono yenu, kama mnaweza. Sawa. Na kama wakiangalia, ye yote ambaye anasimamia maikrofoni hii, ataangalia kwamba inaendelea. Kanda zinaingia?

29 Waamuzi, sura ya 6, aya ya 7. Sasa sikiliza kwa makini, sababu nitarejea kwenye hili katika muda mfupi.

> *Kisha ikawa, hapo wana wa Israeli walipomlilia BWANA kwa ajili ya Midiani,*
>
> *Bwana akamtuma nabii aende kwa hao wana wa Israeli; naye akawaambia, BWANA, yeye Mungu wa Israeli asema hivi, mimi niliwaleta ninyi mkwee kutoka Misri,. . .nikawatoa katika nyumba ya utumwa;*
>
> *. . .nami naliwaokoa na mikono ya Wamisri, na mikono ya wote waliokuwa wakiwaonea,. . .nami niliwafukuza watoke mbele zenu, nami niliwapa ninyi nchi yao;*
>
> *Kisha niliwaambia, Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu; msiiche miungu ya Waamori, ambayo* ninyi *mwaketi katika nchi yao: lakini hamkuitii sauti yangu.*
>
> *Malaika wa BWANA akaenda akaketi chini ya mwaloni uliokuwa katika Ofra,. . .*uliokuwa *mali yake Yaoshi, Mwabiezeri; na mwanawe Gideoni alikuwa akipepeta ngano ndani ya shinikizo, ili kuificha machoni pa* Midiani.
>
> *Malaika wa Bwana akamtokea, akamwambia, BWANA yu pamoja nawe, Ee shujaa.*

> *Gideoni akamwambia, Ee Bwana wangu, ikiwa BWANA yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? yako wapi matendo yake ya ajabu waliyotuhadithia baba zetu, wakisema, Je! Siye BWANA aliyetuleta huku kutoka Misri? ila sasa BWANA ametutupa, naye ametutia katika mikono ya Midiani.*
>
> *BWANA akamtazama akasema, Enenda kwa uwezo wako huu, ukawaokoe Israeli* na mikono ya *Wamidiani. Je! si mimi ninayekutuma?*

30 Iwapo inampendeza Mungu, nataka nichukue somo hapo, juu ya, naamini ile . . . kwenye aya ya 14 hivi, ambapo ilisemwa, *Ikiwa Mungu Yu Pamoja Nasi, Yako Wapi Matendo Yake Ya Ajabu?*

Sasa, sisi sote tunawafahamu Waamuzi, wa Israeli.

31 Na jinsi ambavyo wamewatenda Waisraeli; Wafilisti, Wamidiani, Waamori, na wengineo wameingia kama nzige nao wakala tu walichokuwa nacho, na kukipora na kuendelea. Lakini, umewahi kuangalia, hawakuweza kufanya hilo mpaka kwanza Israeli walipomwacha Mungu.

32 Ibilisi hawezi kuweka unyayo juu yako, kukudhuru, mpaka kwanza uondoke mbele za Mungu. Yakubidi kwanza ukumbuke hilo. Chunguza wakati kitu cho chote kinapotukia, angalia kama uko katika ile Imani, au la, angalia kama uko sawa kabisa na Mungu; basi, kumbuka, Ibilisi hawezi kukudhuru, umo katika Kristo.

33 Na mahali papa hapa, tuliacha punde ile . . . Miaka michache kabla ya hili, palikuwa na nabii mke, Debora; na Baraki. Na jinsi ambavyo alitabiri na kuwaambia la kufanya, na ilikuwa sawa kabisa; Baraki, yule shujaa mkuu wa vita; na jinsi ambavyo waliutunga wimbo, wa ushindi juu ya adui. Lakini mara tu walipotoka kwenye vurugu ile, moja kwa moja wakarudia hali yao ya kwanza.

34 Kama hiyo siyo picha ya kanisa leo! Mara tu linapoondoka katika vurugu moja, huingia moja kwa moja katika nyingine. Lakini muda wa matendo uliwadia. Na ndivyo ilivyo sasa, wakati wa matendo umewadia. Muda ulikuwa umefika, ambapo kuigiza kanisa kumefikia kikomo, kwa Mungu. Hakuna tena kuigiza kanisa. Yatupasa tuingie kwenye jambo lenyewe hasa. Nami naamini kwamba Mungu yule yule ataliweka hili katika mioyo ya watu usiku huu, kwamba wakati umewadia kuacha kuigiza kanisa, kujifanya wa kidini, kuigiza haki, na sasa ni wakati wa matendo.

35 Kama nilivyokuwa ninazungumza asubuhi hii juu ya Uzao mpya ni nini, na jinsi tulivyouendea, hakika hilo bado huzama katika moyo wako. Sasa muda umewadia wa kutenda ambalo unajua kuwa ni Kweli. Huwezi kuenenda kwa imani mpaka

kwanza ujue ambalo unafanya. Yakubidi kwanza ujue ambalo unafanya, kabla hujapata imani ya kulifanya.

36 Mtu mmoja aliniambia wakati mmoja, daktari mashuhuri, alikuwa akizungumzia kuhusu muujiza ambao ulitokea miongoni mwa...mgonjwa. Naye aliniambia, "Mhubiri, je! huamini, kama ungewaambia watu kwenda na kugusa mti au nguzo, jambo lile lile lingelitokea?"

37 Nilisema, "La, bwana." Nikasema, "Kwa sababu huwezi kuwa na imani, katika kugusa mti au nguzo."

38 Imani si legevu hivyo. Yapaswa iwekewe msingi juu ya ukweli fulani unaojulikana. Yakubidi ujue neno juu ya jambo ambalo unaamini, kabla ya kuwa na imani katika jambo hilo. Kwa hiyo kwanza lazima tujue *jinsi gani* na *nini,* mapenzi ya Mungu ni nini, mpango wa Mungu ni nini, na jinsi ya kumkaribia Mungu kwa mpango huo. Ndipo basi twaweza kwenda kwa ujasiri kwenye Kiti cha enzi cha Neema, na kuomba mpango ambao tumeahidiwa.

39 Sasa, walikuwa wakiigiza kanisa. Mara tu walipotoka kwenye vurugu moja...Mungu akawakomboa. Kisha, badala ya hasa kuendelea na kumtumikia Mungu, wakiuona mkono Wake wenye nguvu, walivurugika wakarudi moja kwa moja kwenye mambo ya ulimwengu tena. Na kwa hiyo wakati ulikuwa umewadia, wakati, Mungu alipoagiza ukomo. Na lazima iwe jinsi hiyo.

40 Na nafikiri ni wakati wa kukomesha sasa. Tumelivuruga Neno la Mungu, kufaa kila taratibu zilizopo ulimwenguni. Kila mpango ambao kila mtu amejipangia kutenda. Tumelivuruga Neno kulifanya namna *hii*, na kulivuruga Neno kulifanya namna *ile*, na kulivurugisha namna nyingine kulifanya likubaliane na mpango fulani. Lakini wakati umewadia, kukoma, kuacha kuigiza kanisa kwenu. Wakati umewadia wakati watu wasemapo, "Kama waweza tu kupata Roho wa kutosha, kucheza katika Roho; kama unaweza kupata wa kutosha, kuona nuru mbele ya macho yako; au msisimko ushuke mbio mgongoni mwako, au mtikisiko fulani, mtetemeko fulani, mshtuko fulani, umempata!" Umepata kitu fulani; lakini, nisingesema ulikuwa na nini, hata nitakapoona kumeota tunda la aina gani.

41 Kama tulivyolipitia, asubuhi hii, huwezi kutegemea mtoto mchanga azaliwe mtu mzima. Yapaswa akue kufikia hapo. Nasi hukua katika Kristo, kufikia kimo cha ukamilifu. Kitu fulani... Si mtu aongoke usiku wa leo, na kesho aende akahubiri Injili. Twakua kufikia utu uzima, kufikia kimo cha Kristo.

42 Sasa, tunaona kwamba watu wa Mungu wanapoingia katika shida, Mungu huwapelekea sikuzote nabii mwenye Neno la kweli, kuwatoa. Hakuna wakati ambao watu wa Mungu wanapata kuingia katika shida, bila Mungu kuwapelekea Neno Lake. Na Neno Lake, kama tulivyosikia asubuhi hii, lilikuja

kwa manabii. Na jinsi unavyolijaribu, ni kuchunguza kama linapatana na Neno. Kama linapatana na Neno, basi Neno la Mungu linakuwa hai.

43 Sasa wengi wanaweza kusema, "*Huyu* ni nabii wa kanisa letu." "*Huyu* ni nabii wa kanisa letu." Na hao wawili, wanapingana, mmoja kwa mwingine, hapana budi kitu fulani kina kasoro.

44 Lazima sote tunene kitu kile kile. Basi yabidi tunene, si kinyume, lakini sawa kabisa na Neno hili. Hivyo ndivyo anavyojaribiwa nabii wa kweli, kama ana Neno. Biblia ilisema, "Kama ushuhuda wao haupatani na torati na manabii, hamna Nuru ndani yao." Hilo ni kweli. Yapaswa iwe kulingana na Neno.

45 Naye Mungu sikuzote, katika kila tukio, huwapelekea watu mtumishi wa kweli, nabii wa kweli ambaye ataleta Neno la kweli la Mungu. Na Neno la Mungu ndilo linawakomboa watu, sikuzote.

46 Sasa, kama tungerudi nyuma na tusome aya ya 7 hadi ya 10, twapata, mle ndani, katika hii aya ya 7 hadi ya 10, ya kwamba Israeli walikuwa wamemwacha Mungu, na wamerudi katika ulimwengu tena. Na hapo, akaja kutoka pasipojulikana, hata jina lake halitajwi. Sidhani huyo nabii alikuwa anajali jina lake. Alikuwa anajali jambo moja; Mungu alikuwa amempaka mafuta! Hakujali kama aliwekwa katika kundi moja la madhehebu yao, au kitu kingine, kama alikuwa askofu au askofu mkuu. Kitu pekee ambacho alijali, ilikuwa ni huo ujumbe uliokuwa moyoni mwake. Naye aliwaita watu warudi wakatubu, na kuelewa kwamba Mungu wao alikuwa Mungu mwenye nguvu na Mungu wa ukombozi, Mungu wa miujiza, ambaye aliwatoa katika mikono ya Wamisri, akaifungua Bahari ya Shamu, na kuwalisha jangwani, na Mungu mwenye nguvu ambaye aliweza kuchukua nchi toka kwa mtu mwingine na kuwapa wao. Amina! Huyo alikuwa nabii wa kweli. Alikuwa amepakwa mafuta, naye alikuwa Sauti ya Mungu kwa hao watu. Alinena, kwamba lazima iwe hivyo, kwa sababu wao walikuwa katika shida.

47 Hawa Wamidiani, na Waamori, na kadhalika, wote walikuwa wamekuja na kula nchi yao yote. Na kwa hiyo adui amemkabili, na lazima akabiliwe! Majeshi yao hayakuweza kufanya hivyo, na makasisi wao hawakuweza kufanya hivyo, na makanisa yao hayangeweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, ilihitaji Neno la Mungu, kumkabili.

48 Adui hunena leo. Adui hujaribu kusema kwamba, "Siku za miujiza zimepita. Kwamba, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na huu ni mshtuko tu. Ni kujifanya tu." Kwa hiyo, adui amekaidi, na ukaidi wake lazima ukabiliwe! Njia pekee tuwezavyo kukabili shindano la siku hii, wakati madhehebu wanapowaita watu watoke na—na kuwaweka katika madhehebu *haya*, madhehebu *yale*; huwaachilia wanawake wakate nywele

zao na kujipaka vipodozi; na wanaume, maisha ya kila namna, na kuishi kama wadhamini na mashemasi; na wachungaji kanisani, kwa sababu kuwa na Ph.D au LL.D. ndiyo masharti. Yesu kamwe hakutaka mtu kuwa na hiyo.

49 Masharti ya Yesu yalikuwa, "Ngojeeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mtakapovikwa Uwezo toka Juu, ndipo ninyi ni mashahidi Wangu." Hilo hukabili shindano lake. Hilo lilikabili shindano la adui. Hilo lililikabili katika siku ile. Litalikabili katika siku hii.

50 Sasa nawatakeni muangalie. Katika 7 hadi 10, twaona nabii akija. Toka 1 hadi 7, twaona watu wakianguka. Na kutoka 7 hadi 10, twaona nabii akija na kuwapa watu dawa. Angalia, hatujui alikotokea; hakusema kulikuwa na mtu, Mfarisayo, ambaye kwa muda alikuwa kuhani. Kamwe maisha yake hayakuelezewa. Hao manabii, huinuka toka pasipojulikana!

51 Mwangalie Eliya. Eliya alikuwa wa mwisho, na wa sita, wa manabii wakuu, wa manabii wenye nguvu. Hatujui kitu kuhusu maisha yake. Hatujui shule aliyosomea. Hatujui alitoka katika familia ya namna gani. Kitu pekee tujuacho, kwamba, Mungu alikuwa pamoja naye! Na akatoka, naye akaondoka kiajabu-ajabu kama alivyokuja. Alitoka nyikani kutoka pasipojulikana, na akarudi nyikani, na akapanda gari la upepo, akapelekwa Mbinguni, kwa Moto. Alikuja kiajabu, na akaondoka kiajabu. Hakuwa na misingi ya kitheolojia. Hatujui alitoka wapi, baba yake alikuwa nani, mamake alikuwa ni nani, ndugu zake na maumbu zake walikuwa akina nani. Kitu tu tujuacho, alikuwa mtu wa Mungu. Mungu akimchukua kutoka pasipojulikana, na akamtumia, kisha akamrudisha mahali Fulani, katika Uwepo Wake. Alikuwa mtu wa Mungu.

52 Na hapa anatokea nabii, kwa saa ile, na akawapa Neno la Bwana. Kumbuka, Yeye hakuwapa kamwe theolojia iliyoundwa na mtu. Alisema, "Mimi ni Bwana aliyewaleta kutoka Misri, nilionyesha mkono Wangu wa nguvu, nilionyesha Uweza Wangu." Ningewazia Gideoni alikuwa ameketi papo hapo akimsikiliza! "Mimi ndiye Mungu niliyefanya mambo haya. Nami nimetenda yote haya kwa ajili yenu, na hata hivyo hamkuzitii amri Zangu. Katika yote haya, hamkufanya hilo."

53 Sasa nawatakeni muangalie kitu kingine ambacho kinaweza kukutieni moyo. Mara tu baada ya ujumbe wa nabii yule, Bwana akajitokeza hadharani. Amina! Mara tu alipotoa ujumbe wake, Bwana alitokea chini ya mti. Bwana alikuja, baada ya ujumbe wa nabii, akiketi chini ya mti. Nabii alitoa . . . Watu walianguka, walikwenda kwenye imani zao. Mungu akampeleka nabii Wake. Mara tu nabii alipomaliza ujumbe wake, Bwana alifuatilia ujumbe wa nabii, kwa ajili ya ukombozi!

54 Loo, tunaishi katika wakati mzuri sana! Mara tu baada ya nabii kuondoka hadharani kulitokea nini? Bwana akaja

hadharani! Mara tu Yohana alipoondoka hadharani, Bwana akaja hadharani! Ajabu sana jinsi Bwana atendavyo kazi, lakini Yeye huitenda, hufanya kazi katika njia ya ajabu.

55 Tulisoma Maandiko hapa, ambapo Gideoni, huku anaogopa, nje kwenye shinikizo, akipepeta ngano ya kutosha, kabla ya Wafilisti au Wamidiani hawajamwona. Yeye na baba yake, huko nje wakijipatia chakula kidogo kwa ajili ya chakula chao cha majira ya kipupwe, wakiipepeta, kisirisiri, wasije wakawaona. Sababu, waliingia tu kama nzige, na wakachukua yote waliyokuwa nayo.

56 Hivyo ndivyo Ibilisi atendavyo. Tunaanzisha kanisa dogo, kila kitu kikiendelea vizuri, (Wahubiri wangapi hawajui hili kuwa ni kweli?), hapo wakati tu kila kitu kinaenda vizuri, mjanja fulani wa kale atakuja moja kwa moja miongoni mwa kundi lile na kulirarua vipandevipande. Hilo ni kweli, kulinyakua kanisa moja kwa moja toka kwa mtu, kama anaweza kufanya hivyo. Unaona, huyo ni Ibilisi, anakuja kama nzige na kuchukua kilichotolewa. Sasa wakati . . .

57 Hakika Gideoni alikuwa mtu wa Kimaandiko. Malaika wa Bwana alipomwambia . . .

58 Na kama ukiangalia, haikuwa Malaika wa Bwana hapa. Ilisema, "Na Bwana," herufi kubwa za B-w-a-n-a. Haikuwa Malaika. Ilikuwa Mungu. Ilikuwa m—mwili wa kiungu katika mtu, katika umbo la Mungu, kama ilivyomtokea Ibrahimu kule nyuma nyikani, na ilionekana kama mwanadamu. Basi kwa hiyo, akiwa Mjumbe, Yeye alikuwa Malaika wa Bwana.

59 Na Yeye alimtokea. Kisha akasema, "Ee shujaa," akasema Yeye atamchukua, na kuwaokoa Israeli kwa yeye.

60 Naye Gideoni aliuliza swali lile. Jinsi huyo alivyokuwa mtu wa Kimaandiko! Mungu humjia mtu wa namna hiyo, mtu ajuaye. Gideoni akasema, "Kama Mungu yu pamoja nasi, kama Wewe ndiye Mjumbe, basi yako wapi matendo ya ajabu ambayo nabii alituambia?" Alijua, kila alipokwenda Mungu, miujiza Yake ilimfuata. Alijua kwamba po pote alipo Mungu, miujiza ipo.

61 Na wawezaje kumtazamia Mungu, leo, kutenda kazi miongoni mwa watu ambao hata hawaamini katika miujiza? Yawezekanaje?

62 Naye alimwita, "shujaa." Kasema, "Sasa, kwa hili, utawaokoa Israeli."

63 Sasa, huyo alionekana kama mtu ameketi pale, na ilikuwa Mwanadamu. Na alimtazama Yeye, akasema, "La, Bwana wangu, ikiwa Mungu yu pamoja nasi, basi mbona taabu hizi zote zimetupata? Na yako wapi matendo ya ajabu ambayo tunaambiwa habari zake? Yako wapi mambo ambayo Mungu alikuwa akiyatenda?"

64 Sasa hiyo ndiyo njia nzuri ya kujua kama mjumbe ni wa kweli, au la. Kama yuna namna ya utauwa, atakana Nguvu zile hutenda ile miujiza. Kama yeye ni mjumbe toka kwa Mungu, hatazungumzia jambo hilo tu, lakini atakuwa nayo; kuifanya, na kuonyesha kwamba Mungu yule ambaye anazungumzia habari zake yu pamoja naye na ndani yake.

65 Akasema, "Kama Mungu alikuwa pamoja nasi, yako wapi matendo Yake yote makuu ya ajabu? Sababu, tunasikia..." Sikilizeni jinsi Gedioni alivyokuwa wa Kimaandiko. Kwa namna nyingine, alisema, "Kama...Tunasikia kwamba Mungu ni Mungu mkuu wa matendo makuu. Yeye ni Mungu mkuu wa miujiza. Na kama Yeye yu upande wetu, na kama Yeye yu pamoja nasi, na ni Yeye yule jana, leo na hata milele, naweza kuiona wapi miujiza Yake? Naweza kumuona Mungu huyu wapi akitenda kazi? Yuko wapi, kama Yeye yu upande wetu?"

66 Yule shujaa aliweza kurejea kwenye lile Neno la kale, na kujua Hilo ni sahihi, kwa sababu alijua hili, kwamba, Mungu ni Kiumbe cha kimbinguni. Na po pote kilipo Kiumbe cha kimbinguni, Yeye atatenda ishara za kimbinguni, kwa sababu cha kimbinguni kiko ndani Yake. Huwezi kulikwepa.

67 Unawezaje kusimama kwenye upepo, bila upepo kuvuma? Wawezaje kuingia majini, bila ya kulowa? Maji ni chepechepe. Hivyo ndivyo yalivyo.Ni chepechepe! Na uingiapo majini, utalowa. Sawa!

68 Na uingiapo kwenye Uwepo wa Mungu, yule wa kimbinguni, kutakuwa na ishara za kimbinguni na kazi za kimbinguni za Mungu wa mbinguni.

69 Kwa hiyo alisema, "Wapi yale matendo, yako wapi yale matendo ya ajabu, kama Mungu yu pamoja nasi?"

70 Utukufu! [Ndugu Branham anapiga makofi, mara nne—Mh.] Basi! Unaona, alipo Mungu, miujiza ipo. Alipo Mungu, ishara ya Mungu ipo. Unaona?

71 Na Gideoni, wa Kimaandiko sana, akasema, "Mambo haya yako wapi?" Kwa maneno mengine, hivi, "Mimi ni mtu, labda wa umri wa miaka hamsini," angesema. "Na nimewasikia wakizungumza kuhusu Mungu ambaye alitenda maajabu. Nami nimeenda kanisani, na nimewaamini makasisi. Pia ninaamini manabii. Na ninaamini Neno lililoandikwa, magombo yote ya chuo. Nami nilisoma katika hayo magombo ambapo, Mungu, alipokuja miongoni mwa watu Wake, kitu fulani kilitendeka." Na Gideoni hakujua ila kwamba huyo alikuwa mtu ameketi chini ya huu mwaloni. Amina! Hayo ndiyo aliyojua tu, Yeye alikuwa mwanadamu. Akasema, "Sasa, kama Mungu yu pamoja nasi, matendo yake ya ajabu yako wapi? Tunataka kuyaona."

72 Jinsi hilo lilivyo la Kimaandiko! Kwa sababu, alipo wa kimbinguni, Mungu na ishara Yake itakuwa pamoja Naye. Alipo Mungu, ishara ya Mungu ipo pamoja na Mungu. Twajua hilo.

Kama yupo katika watu Wake, watatenda ishara Zake. Sawa sawa kabisa.

73 Hilo ndilo swali alilokuwa nalo Gideoni, "Ndiyo, Mungu yuko wapi? Kama kuna Mungu, kama Mungu yuko pamoja nasi, basi hebu nione ishara Yake ilipo. Twaambiwa kwamba Yeye huzifanya. Na iwapo kazi hii kuu ipo mbele yangu . . . "

74 Labda yule Mzee aliposimama pale, alionekana kama Mtu mzee. Biblia ilisema alikuwa na fimbo mkononi Mwake. Endelea kusoma, sura ya 6, utakapoenda nyumbani, au wakati fulani kesho.

75 Alikuwa na fimbo mkononi Mwake; Mzee, alionekana hivyo, akiketi chini ya mti. Naye akamwita, "shujaa." Naye akasema kwamba Mungu angetenda kitu hiki. Na Yeye akasema, "Mungu yu pamoja nawe."

76 Akasema, "Basi matendo Yake ya ajabu yako wapi? Kama Mungu wa mbinguni yupo hapa, kazi za Mungu za mbinguni ziko wapi?"

77 Hilo lingeweza kusemwa kwa urahisi usiku wa leo miongoni mwa makanisa yetu. "Yuko wapi Mungu yule ambaye aliishi wakati mmoja? Je! Alikufa? Ameenda zake? Ana shughuli? Amekwenda safari?" La, bwana.

78 Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na kama tukisema sisi tu wa Mungu, basi hebu na tuone alipo Mungu. Hebu na tuone ishara za Mungu. Kama Maskani hii ni ya Mungu, hebu na tuone Mungu akitenda kazi miongoni mwetu. Na tuone watu wakizaliwa katika Ufalme. Na tuone maisha yakinyooshwa. Hebu tuone wagonjwa, na vipofu, viziwi, na tuone kazi Zake kuu zikitendwa. Mungu katikati yetu!

79 "Kama Mungu yu upande wetu, matendo Yake ya ajabu yako wapi? Aliuliza hilo swali.

80 Sasa, kama Mungu yu pamoja na watu Wake, na katika watu Wake, hawezi . . . mtu huyo hawezi kujizuia ila kufanya kitu kile kile Mungu alichofanya. Kwa sababu, si yule mtu tena, ni Mungu katika mtu yule. Kama mtu huyo akitenda dhambi, basi Mungu hayupo katika hilo. Kama akiupenda alimwengu, basi Mungu hayupo katika hilo. Nasi twajua kwamba Mungu hachukuliani na dhambi. Sasa nitawapa Andiko kwa hili, katika muda mchache tu.

81 Yesu, alipokuwa duniani; Yeye aliulizwa swali lile lile. Walitaka kujua, "Wewe, ukiwa Mwanadamu, na wajifanya Mwenyewe Mungu?"

82 Alipomponya yule mtu mwenye kupooza, Yeye alisema, "Usamehewe dhambi zako."

83 Akasema, "Sasa ngoja kidogo! Wewe, ukiwa u Mwanadamu, na unasamehe dhambi?"

84 Akasema, "Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anao uwezo duniani, kusamehe dhambi au kuponya; ni kipi rahisi, 'Chukua kitanda chako uende,' au—au kusema, 'Usamehewe dhambi zako'?" Ndipo akamzungumzia yule mtu, naye akainuka akaondoka akaenda zake.

Nao Mafarisayo wakamswali.

85 Naye Yesu akasema, "Kama hamniamini Mimi, aminini ishara nizifanyazo." Unaona, waliambiwa kwamba kungekuwa na Nabii, kama Musa, atakayeinuka, naye angekuwa Masihi. Naye alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi; nimekosea. Lakini kama nikitenda kazi za Baba Yangu, nanyi hamniamini Mimi, basi aminini zile kazi. Kazi zinafanya nini? Zinakuambia Mimi ni nani. Zinanishuhudia Mimi. Ni shahidi Wangu. Si vitambulisho vyangu kwamba ni wa kanisa la Kipresbiteri au Kipentekoste, naweza kuonyesha kadi yangu ya ushirika; lakini kazi nizifanyazo, ishara za Mungu, ishara za Masihi, ndizo zinazonishuhudia Mimi."

86 Yesu alisema, katika Yohana Mt. 14:12, kama mngeandika Maandiko. Yohana Mt. 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Amina!

87 Ni kitu gani, ndugu zanguni? Kama Mungu yu upande wetu, matendo yake ya ajabu yako wapi? Kama Mungu yu pamoja nasi, basi tuna nini? Kuna kasoro mahali fulani! Ndiyo.

88 Yesu alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, yale nisemayo; angalieni kile kinachonishuhudia Mimi, kwani ndizo zinazonishuhudia Mimi. Bwana Mungu wenu alisema, 'Atainuka nabii kama Musa. Na ye yote ambaye hatamsikia Nabii huyu, atakatiliwa kutoka miongoni mwa watu.' Masihi alikuwa awe na ishara inayomfuata Yeye. Na kama ishara ile ya Masihi haifuatani Nami," alisema Yesu, kwa maneno mengine, "basi msiniamini Mimi. Lakini ikiwa ishara ya Masihi inanishuhudia Mimi, basi aminini ishara hiyo. Sababu, kama mkidhani nimekosea, ishara hiyo ni sahihi kwa sababu ni ya Kimaandiko." Haleluya!

89 Hapo ndipo ambapo Gideoni alipotaka kufikia. Hapo ndipo Gideoni alikuwa amesimamia. "Loo, kama kuna Mungu aliye pamoja nasi, tunataka kuona ishara ile kwamba Yeye ni Mungu, kwamba Yeye ni Mungu yule yule, kwa sababu Yeye atafanya ishara zile zile." Mungu alifanya nini?

90 Gideoni alisema, "Ngojea, na nitaleta kidogo, sadaka." Naye akatoka akachinja ng'ombe, au mwana-kondoo, akamchemsha. Akaleta mkate na akaleta mwana-kondoo, akamlaza chini.

91 Yule Malaika akasema, "Nitangojea hapa." Hakikisha mambo yote. Yajaribuni kwa Neno. Naye akasema, "Nitangojea hapa," labda masaa mawili au matatu.

92 Gideoni akaja na mchuzi na mkate, na nyama. Yule Malaika akasema, “Sasa utaelewa kwa hili. Hili litalihakikisha.”

93 Akamwaga ule mchuzi ardhini, kwa sadaka ya kinywaji. Kisha akachukua ule mkate na ile nyama na akaiweka juu ya mwamba ambapo alikuwa akipepetea.

94 Basi akachukua ile fimbo toka mkononi Mwake, kama Mzee, fimbo, kisha akaigusa. Basi alipoigusa, moshi ulitoka, na sadaka ikateketezwa. Ilikuwa ni nini? Alimrudisha kwenye Maandiko, kuhakikisha Yeye alikuwa ni nani, Mungu yule yule aliyekuwa pamoja na Eliya katika Mlima wa Karmeli!

95 Mtu yule Mmoja niliyezungumzia habari Zake asubuhi hii! Uwekapo nafsi yako juu ya madhabahu Yake ya shaba ya hukumu, kunatukia nini? Kama Yeye ni Mungu yule yule, atachukua sadaka hiyo! Umeitoa kwa uaminifu kwenye madhabahu Yake, ataiteketeza Kafara ile na ulimwengu utakuacha. Moshi tu ndio utakaoanguka. Kafara itakuwa imekwenda. Ndiyo.

96 “Kama Wewe u Mungu, na Wewe ni Mungu wa Biblia, ambaye baba zetu hutuambia kwamba alitenda maajabu, hebu nikuone Wewe ukitenda maajabu, au hebu nione namna fulani ya muujiza, nipate kujua kwamba Mungu amekutana nami.”

97 Sasa hebu niseme hili. Kama Mungu bado yuangali Mungu, kama Mungu ni Mungu yule yule wa siku zilizopita, haikulazimu kwenda kupeana mikono na mhubiri, haikulazimu kwenda kuandikisha jina lako kwenye kitabu. Mambo hayo yote ni sawa; siyapingi. Kisha unarudi na kuwa mfuasi wa kanisa, na jina lako limeandikwa kitabuni, nao wanakupa barua, na unaichukua. Mara tu kitu fulani kikienda kombo humo, unalipuka kama sijui kitu gani, kisha unaichukua kwenye kanisa lingine. Na mara kitu fulani kikienda kombo huko, ndipo utaichukua kwenye kanisa lingine. Unaona, kwanza hukufanya haki. Kama Mungu yuangali Mungu, iweke nafsi yako yenye dhambi kwenye madhahabu Yake, Naye ataigusa kwa Neno Lake na Uwezo Wake. Na ulimwengu utakuwa umekutoka, kisha utakuwa kiumbe kipya, kama Yeye yuangali Mungu.

98 Alikuwa Mungu wa Agano la Kale. Alikuwa Mungu wa Agano Jipya. Ni Mungu yule yule leo. “Jana, leo, na hata milele.”

99 Na unajua basi, chini katika moyo wako, kwamba kazi isiyo ya kawaida imekwishafanywa na Kiumbe kisicho cha kawaida. Ambapo kwanza ulikuwa unakunywa pombe na kuvuta sigara, na kudanganya; nanyi wanawake mliupenda ulimwengu sana, mliendelea kujipaka vipodozi vyenu, na nywele zenu ndefu . . . au nywele fupi, na kufanya mambo mengine mliyofanya, na mnaona kwamba kitu fulani kimetukia, kwamba pepo wote wa kuzimu hawangeweza kukufanya ulifanye tena. Kitu fulani kilitukia, Mungu wa maajabu alitenda kazi!

100 Yeye alifanya nini? Alibadili moyo wako mpotovu, alibadili tamaa zako, alibadili asili yako. Neno la kimbinguni, kwa Mungu wa mbinguni, alikifanya kiumbe cha wakati kuwa kiumbe cha Milele. Amina! Alikuondolea ulimwengu, na akamuweka Kristo ndani yako, tumaini la Utukufu. Nawe umejazwa na Roho Wake, na u tayari kukutana Naye.

101 Mungu akiwa Mungu, yako wapi maajabu Yake? Kama Mungu yu pamoja nasi, maajabu Yake yako wapi?

102 Kama Mungu yu pamoja na kanisa la Kimethodisti, kwa nini hao wanawake wote wangali wanakata nywele? Kama Mungu yu pamoja na kanisa la Kibatisti, basi kwa nini mchungaji bado anavuta sigara, wengi wao? Kwa nini wangali wanakana Nguvu za—za Mungu, kuponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kunena kwa lugha, na kutafsiri lugha, na vipawa vya unabii? Kwa nini bado wanalikana, kama Mungu wa Agano la Kale na Mungu wa Agano Jipya bado ni Mungu yule yule? Kama Mungu wa Agano Jipya, Roho Mtakatifu, bado ndiye Mungu Wapentekoste wanayemdai, kwa nini hawavibomoi viambaza vyao vinavyowatenganisha, na kugombana mmoja na mwingine, na kuwa Wakristo waliozaliwa mara ya pili? Hakika. La, mmoja hata hatazungumza na mwingine. Unaona, kafara bado haijateketezwa. Wanapata mishtuko, wametenda yote . . . Katika nyakati zilizopita, chini ya ibada ya sanamu, wamepata mishtuko.

103 Lakini Mungu wa—wa Biblia, huyo ndiye Mungu, Yeye yule jana, leo, na hata milele, huuteketeza ulimwengu na tofauti zote, kutufanya viumbe vipya katika Kristo. Ndiyo. Yesu alisema, "Hizi hushuhudia na kuwaonyesha Mimi ni nani."

104 Jambo lenyewe ni kwamba, sababu ya kuwa na mambo yote haya, ni kwa sababu bado tunaruhusu tofauti za kimadhehebu, kanuni za imani, ugomvi, kupendwa na watu, na pepo wa dunia, yatupofushe na Ukweli halisi wa Mungu. Hiyo ni kweli.

105 Watu wengi wamedanganyika, katika kumpokea Roho Mtakatifu; kama nilivyosema, wanayo mafundisho leo, kama mavazi ya Eliya, na—na mambo haya yote, Wana wa Mungu waliodhihirishwa, na imani hizi zote mbalimbali, na kadhalika, ulimwenguni leo. Watu kwa upofu huangukia hapo, na kuingia katika namna fulani ya mshituko, wakainuka wakiwa na roho ya kiburi, kutojali, ya ugomvi, hasira kali. Huyo siye Roho wa Mungu. Bado wanaendelea, nje ya utaratibu, hawajui utaratibu wa Kanisa ni nini, hawajui jinsi ya kuwa na tabia njema katika nyumba ya Mungu, hawana adabu, la, ufidhuli chungu nzima, ha—hawamjali Mungu, yote wanayofikiria tu ni "kanisa langu." Inaonyesha walipokea roho ya kanisa, na wala si Roho wa Mungu; sababu Roho huondosha hayo yote ndani yako, akayachoma moto. Hakika.

Unaona, wao husema, “Yuko wapi Yeye?” Yaani, tuna haki kufanya hivyo.

106 Lakini, angalia, kama mawingu yananing’inia juu ya jua, wakati wote jua linawaka. Kitu tu ambacho kinalizuia lisikuangazie, ni mawingu. Na kama ukiyaondoa hayo mawingu, jua litakuwa likiangaza. Amina.

107 Ndugu, tuondoke kwenye dhambi zetu zote na mashaka yetu, na wasiwasi wetu, Mwana ameangaza tangu Siku ya Pentekoste! Roho Mtakatifu yu mkuu leo kama Yeye alivyowahi kuwa. Lakini madhehebu yetu yamelifunikiza Neno la Mungu, katika kusema, “Ni kwa siku nyingine. Loo, hilo, uponyo wa Kiungu, utakuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. “Au, “Uponyo wa Kiungu ulikuwa wa zamani *zile*. Si wa siku hii.”

108 Anawezaje Yeye kuwa yeye yule jana, leo, na hata milele, na halafu uponyo wa Kiungu usiwepo? Yawezekanaje ule Uweza, yawezekanaje . . . Biblia imeweka katika utaratibu, “Kwanza mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji, kwa thibitisho kwamba Injili bado ingali hai.” Na Mungu huwapeleka moja kwa moja miongoni mwetu, nasi twalipa kisogo. Mungu hashindwi, watu ndio wameshindwa.

109 “I wapi miujiza miongoni mwetu? Iko wapi?” Mungu alikuwa akizungumza na mtu huyu, akimtayarisha kwenda.

110 Ondoa mawingu, jua linawaka sikuzote. Hilo ni kweli. Mashaka yanapoondoka, na mambo yamewekwa sawa, miujiza itakuwepo hapo bila shaka kama Mwana alipo hapo.

111 Jua, kwa amri ya Mungu, huwaka kila siku. Lipo hapo kwa sababu Mungu ameliamuru liwepo. Na kadiri kuna mchana na usiku, jua litaning’inia pale. Hakika. Hulioni wakati wote, kwa sababu mawingu yamelifunika; ukungu, mawingu, yaliyo chini au juu, hulifunika. Lakini sikuzote lipo hapo, unaona.

112 Na jambo tu mnalotaka kufanya, kuona miujiza leo, kama mnataka kuona muujiza wa Mungu, ondoeni tu mashaka yenu yote. Ondoeni kanuni zenu za imani, ondoeni madhehebu yenu yote, na huyo hapo Mwana ananawiri mwenyewe.

113 Ni Amri ya Mungu, kwani lilisema, “Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa hiyo, maadamu Yeye atakuweko sikuzote, Yeye yupo! Hakuna swali juu yake, Yeye yupo! Matendo ya ajabu yako wapi? Kitu gani kinazuia matendo ya ajabu? Mungu alimpeleka Kristo, Kristo yu hai milele! “Po pote wakusanyikapo wawili au watatu kwa Jina Langu, Mimi nitakuwa katikati yao.” Amina! “Tazama, Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” Huyo hapo, ahadi Yake!

114 Kuna kitu gani basi? Tumeachilia mawingu ya mashaka, choyo, hasira, ubinafsi, madhehebu, na mambo mengine, yatuvamie, yatuvamie na kutuondoa kwenye Neno, kusema,

"hayo yalikuwa ni ya mahali pengine," tukimkana Kristo, tukiukana ubatizo wa—wa Bwana, wa Roho Mtakatifu, tukiukana Ubatizo wa Kikristo wa Jina Lake Yesu Kristo, mambo mengine, mambo ya namna zote, ambayo kanuni za imani zetu zimetuondoa kwenye Biblia. Lakini katika . . .

115 Je! Si ni jambo la ajabu, muujiza, kwamba mbele ya yote hayo, Ndugu Way, mbele ya madhehebu yote, mbele ya watoa lawama wote, Biblia haibadiliki? Ilistahimilije tufani? Mungu amekusudia kumhukumu kila mtu kwa Biblia. Na Biblia ni Neno, nalo Neno ni Kristo. Kila mmoja, kila mtu atahukumiwa kwa Hilo.

116 Ondosheni mawingu, basi kinachotukia ni kwamba, jua lipo hapo tu; kitu pekee unachopaswa kutenda leo si eti kusema, "Ee Yesu, njoo uniponye! Ee Yesu, nipe Roho Mtakatifu!" Ondoa tu mawingu, tayari Yeye yupo hapo! Alikuja miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, na Yeye bado yupo! Na Yeye sikuzote atakuwa hapo! "Naishi milele na milele, yeye yule jana, leo, na hata milele." Hilo ni kweli!

117 Sasa, Gideoni na watu wale pale, kabla ya kuweza kuona, au kuweza kwenda, kuona maajabu haya ya Mungu, palikuwa na masharti ya kutimiza. Kukutana, kuona Nguvu za maajabu, iliwabidi kuamini. Pia iliwabidi wao waamini na kutii Neno la nabii, kuona miujiza ya Mungu. Sasa, kumbuka, kabla ya kuona maajabu, iliwabidi kutii alichonena nabii.

118 Na kabla ya kuweza kuona miujiza ya Mungu, yatubidi kutii wanayosema manabii. Biblia ni Nabii, kwetu. Hilo ni kweli!

119 Iwapo mtu, haidhuru jinsi gani yeye anajiita nabii wa Mungu, wa Kibatisti, Kimethodisti, Kipentekoste, hata awe nani, hata ajiite nini, kama Neno hili haliishi ndani yake, yeye si nabii. Aweza awe ni nabii, lakini, wa uongo. Manabii wa kweli hunena kuhusu Neno hili la kweli, na kisha humweka Mungu kuwa Mungu yule yule kabisa, Uwezo ule ule, Maneno yale yale, kila kitu kile kile, Neno la kweli.

120 Sasa, iliwabidi kuamini. Iliwabidi kuamini Neno la nabii na kulitii, kabla wao hawajaweza kuona maajabu ya Mungu.

121 Na leo, huwezi kwenda hapa ukiwa na mambo ya bandia, ukisema kwamba "Yesu siye yeye yule jana, leo, na hata milele; siku za miujiza zimepita; na hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu," na kutazamia kuona maajabu ya Mungu. Yakubidi kutii Hilo. Na unapotii Hilo, Mungu hujishughulisha na yale mengine.

122 Kama ungeweza kuyarudisha nyuma mawingu yote, jua tayari liko hapo. Huning'inia tu hapo. Jua halisogei, tunaambiwa. Jua hubakia mahali pale pale.

123 Naye Kristo hudumu! Na hilo ni sahihi. Sisi hujiondoa Kwake, lakini Yeye haondoki. Hilo ni kweli. Jambo tu likupasalo

kutenda ni kujigeuza na kumkabili Yeye mara moja, na unaona litakalotukia. Mgeukie Kristo! Usiligeukie kanisa, usiigeukie imani, usiyageukie majina ya heshima; mgeukie Kristo! Unaona, usigeukie seminari; ligeukie Neno! Kristo ni Neno. Hakika, ni Neno. Hilo ni sawa hasa.

124 Tii Neno, kwetu sisi. Iliwabidi kutii Neno. Na, kwetu sisi, yatubidi kulitii Neno.

125 Kama ungependa kujua hilo, nina Andiko limeandikwa hapa, kasema, "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo lote." Unaona? Ilikuwa nini? Kama Neno la Mungu liko ndani yetu, na linakaa humo, Hilo huzungumza Lenyewe. "Ombeni mtakalo lote, nanyi mtapewa." Sasa, hilo linapatikana katika Yohana 15:7, kama unataka kuliandika. Unaona, Yesu alisema, "Ninyi mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakikaa ndani yenu."

126 Siyo leo u kitu *kimoja*; kesho yake, kitu kingine; na kurudi nyuma, na juu *hapa*, na chini *hapa*, na chini *kule*. Inaonyesha hujapata cho chote, kwanza.

127 Ama, unasema, "Nilinena kwa lugha." Vizuri, lakini wewe bado hujapata kitu cho chote. Unaona? Wasema, "Nilicheza katika Roho." Vema, lakini bado sijui ni roho ya namna gani uliyocheza ndani yake. Unaona?

128 Kama uko kwenye jambo moja, siku moja; na wiki ifuatayo, jambo jingine; na kigogota mwingine mdogo ajapo, akidonoa kwenye mti mtupu ndani, unamuendea mbio na mwingine upande huu, ni kuzurura misheni kwa misheni, hujui u mali ya nani, basi Kristo hakai ndani yako. Maneno Yake hayapo hapo. Kwa sababu, Hayo ni imara, hutageukia giza kamwe!

129 Kama nilivyohubiri hivi majuzi juu ya "*Kitendawili*," wakati Yoshua aliposimamisha jua. Becky nyuma huko, alisema, "Baba, asingeweza kusimamisha jua," alisema, "dunia ingesimama. Alisimamisha dunia."

130 Nikasema, "Alisimamisha jua." Mungu hafanyi makosa yo yote katika Biblia Yake.

131 Kasema, "Angewezaje kusimamisha jua, jua hata halisogei? Jua husimama kimya."

132 Nikasema, "Lakini hicho, hicho chombo cha angani huko nje, sicho Yeye alikuwa akikizungumzia. Jua hili ambalo lilikuwa linasafiri na kutoa mwangaza duniani, hilo ndilo jua alilosimamisha."

133 Sijui Mungu alitenda nini, kulifanya litimie, lakini Yeye alisimamisha jua. Jua lilikuwa likienda *hivi*, jua duniani, kurudishwa nuru ya jua. Hicho chombo cha angani nje huko, hatungeweza kuona katika maili milioni kadha yake, au maili milioni kadha. Lakini nuru ya jua, ambayo ilikuwa ikisafiri juu ya uso wa nchi, toka mchana hadi usiku, hiyo ndiyo Yoshua

aliamuru kusimama kimya; nayo ikasimama. *Kitendawili* ni jambo ambalo "haliaminiki, lakini ni kweli." Kwa hiyo, hilo haliaminiki, lakini hata hivyo ni kweli.

134 Mungu anawezaje kumchukua mwenye dhambi, mwenye kiburi, mwenye hasira kali sana, mtu wa ugomvi, na kumfanya mtakatifu wa Mungu? Anawezaje Yeye kumchukua mwanamke ambaye ni mwovu, mpaka hata mbwa wasingemgeukia huko mitaani, na kumfanya kuwa mtakatifu wa Mungu? Siwezi kukuambia. Lakini amelitenda! Ni kitendawili. Ndivyo hakika! Kazi kuu zote za Mungu ni kitendawili.

135 "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote, nanyi mtatendewa." Yohana Mt. 14 au Yohana Mt. 15, samahani, Yohana Mt. 15:7. Sawa.

136 Turudi Mwanzo, kwa muda kidogo. Ilibidi Nuhu kutimiza masharti. Ilimbidi Nuhu kuamini Neno la Mungu, na kulitekeleza, kabla ya kuona muujiza wa Mungu. Hilo ni sawa. Nuhu, yule nabii mkuu wa Mwanzo, ilimpasa aamini Neno la Mungu na kulitekeleza, kabla ya kuona muujiza wa Mungu. Haikuwa imenyesha kamwe, unajua, hakujawahi kuwa na mvua kamwe.

137 Na unafikiri wanatuambia nini? Kwamba, wakati ule ulikuwa wakati mkuu kuliko tunaoishi sasa, katika sayansi. Hatuwezi kujenga piramidi tena, au sfinksi. Hatuna njia ya kutengeneza mumiani, hatuwezi kuyakausha maiti jinsi hiyo. Hatuwezi kuweka rangi katika nguo, kudumu, kama walivyofanya nyuma huko. Hata hatuna mambo hayo. Na hilo ni jambo ambalo sayansi yetu ya kisasa haiwezi hata kugundua. Lakini wao walikuwa nayo!

138 Hatuna—hatuna wahandisi kama waliokuwa nao. Piramidi hiyo kuu huko Misri ni kamili kabisa hapo katikati ya dunia, haidhuru jua liwepo wapi, hakuna kamwe kivuli kando yake. Hatungeweza kujenga jengo kama hilo. Hatujui jinsi ya kulijenga. Wala tusingeweza kujenga piramidi. Na juu ndani huko, juu kuzungukia mawe ya kifuniko na ndani humo, ikisimama karibu nusu ya urefu wa jengo la mjini juu hewani, kuna mawe yaliyo na uzito wa tani bilioni kadha, tani mia kadha, hasa, yakining'inia juu kule. Mitambo yote tuliyo nayo duniani haingeweza kuyainua kule juu.

139 Wananiambia itahitaji magari makubwa kumi na sita, kuubeba mguu mmoja wa ile sfinksi. Waliupelekaje kule? Ilitukiaje? Walikuwa wanasayansi hodari sana!

140 Na unadhania walimwambia nini mtu, mshupavu wa dini, aliyedhaniwa nabii, ambaye alisema, "Kuna maji yatakayotoka angani?"

141 Naweza kuwasikia wakisema, "Tunachukua vyombo vyetu, na kuvirusha kufikia hadi kwenye nyota, na hapana hata tone moja la maji katikati ya hapa na huko. Iko wapi?"

142 Nuhu angewajibu hivi, "Mungu aliniambia, 'Itanyesha.'" Hilo latosha. Basi. Mungu alisema itatendeka, kwa hiyo hilo ndilo tu litakalotendeka. Vema. (Yanibidi niharakishe; ndugu wengine wanangojea.) Hapa, Nuhu, alisema, "Itanyesha."

"Unajuaje?"

"Ni Neno la Bwana. Ni BWANA ASEMA HIVI."

143 "Utafanyaje juu ya jambo hilo, Nuhu, utazurura na kuhubiri hilo?"

"La, bwana. Nitajitayarisha kwa ajili yake." Unaona?

"Loo, huo utakuwa muujiza! Siku za miujiza zimepita."

"Tulieni tu, mtaona baada ya muda mchache." Ndiyo, bwana.

144 Alitenda nini? Alijenga safina kabla ya mvua kunyesha. Alikuwa akifanya nini? Akitekeleza ile ahadi. Amina. Najisikia hali ya kipentekoste sasa hivi, najisikia mwanadini!

145 Ndiyo, amini Neno asemalo Mungu, tenda kulingana na ahadi, bila kujali linalotendeka, ni juu ya Mungu kutenda mengine yote. Anza tu kugonga mawingu! "Wekeni kando kila uzito uwazingao." Wekeni kando mashaka yenu yote, hofu zenu, madhehebu yenu, kanuni zenu za imani, na kila kitu ambacho ni kinyume cha Neno. Yesu Kristo ni yeye yule tu jana, leo, na hata milele. Wekeni kando tu kanuni zenu za imani, wekeni kando madhehebu yenu, wekeni kando mashaka yenu, wasiwasi wenu wote kando, na muendelee tu. Muda si muda, uta—utaondoa kipande chako kikubwa cha mwisho, na Yeye atakuwa amesimama hapo. Utakutana na Yeye.

146 Nuhu alisema, "Nitakapokwisha kujenga safina, Yeye atakuja. Mvua itaanza kunyesha!"

"Siku ile utakapomaliza kujenga safina?"

147 "Kama itakaa miaka hamsini, nitakuwa nimeketi katika safina, nikiingojea. Inakuja, maana Mungu alisema hivyo!"

148 Unaona, jambo la kwanza, ilimbidi ajiandae. Alijua kwamba Mungu alikuwa Mungu wa maajabu, kwa hiyo hakuweza kumtilia Yeye shaka. Mungu alikuwa amenena naye, naye alilijua hilo.

149 Mungu anapokuzungumzia, kutoka kwenye Neno Lake, unajua hilo katika moyo wako. Ulimwengu wote unapokutoka, na mambo ya ulimwengu yamekufa, unajua. Wakati, kama unaupenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu, bado unajua, moyoni mwako, hauko sahihi. Ni kweli. Kwa hiyo, wakati kila kitu kimeondoka, basi hakuna la kutenda isipokuwa kukutana na Mungu. Yeye atakuwa amesimama hapo. Yeye yuadumu.

150 Kama vile jua, j-u-a, vivyo hivyo M-w-a-n-a hudumu yeye yule jana, leo, na hata milele. J-u-a hilo ambalo huwaka, ndilo jua lile lile lililowaka katika Mwanzo, jua lile lile

lililomwangazia Eliya mlimani, jua lile lile lililoshuka siku ya kusulubiwa. Haleluya! Hudumu vivyo hivyo. Na Mwana yule yule wa Mungu, ni yeye yule jana, leo, na hata milele; Uweza ule ule, upendo ule ule, yeye yule katika ishara.

151 Ni nini, leo, ishara ya Mkristo? "Loo, anaenda kanisani, huandikisha jina lake kwenye kitabu, ana barua." Hiyo si ishara aliyosema Yesu.

152 Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kwa Jina langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya. Kama wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

153 Kama Mungu yu pamoja nasi, ishara Zake ziko wapi? Hakika, rudini kwenye Neno Lake, ishara zitajishughulikia zenyewe mara tutakaporudi kwenye Neno.

154 Nuhu, kabla ya kuona maajabu ya Mungu, kama Gideoni alivyotaka kuulizia hilo, ilimbidi kwanza atekeleze Neno la Mungu. Ilimbidi Gideoni atekeleze Neno la Mungu.

155 Kila mtu yambidi atekeleze Neno la Mungu. Kabla sijaweza kusema kwamba kuna Mungu, ilinibidi nitekeleze ahadi Yake, ndipo alipojidhihirisha. Kama unataka uponyo, mwamini Yeye! Tekeleza Neno Lake, itatimia.

156 Musa, kabla ya kuona maajabu ya Mungu, ilimbidi kwanza kutekeleza Neno la Mungu. Yeye alijua amemsikia mama yake akisema amezaliwa kiajabuajabu, alifichwa kwenye majani. Mama alimwambia kwamba Mungu alimwita na amemchagua.

157 Naye akafikiri, "Vema, mimi nikiwa mwanajeshi mzuri, naweza kutoka hapa tu na kumuua—kumuua Mmisiri huyu na kumficha katika vumbi. Na ninaweza kufanya cho chote ninachotaka. Hicho ndicho tu kinachohitajika." Lakini, unaona, hilo ndilo alilokuwa anajaribu kufanya. Hilo ndilo wazo lake. Hajamwona kamwe huyo Mungu akitenda—akitenda muujiza kumdumisha katika wakati ule.

158 Lakini siku moja, baada ya yeye kuwa na umri wa miaka themanini, alikuwa akichunga kondoo, ameshika njia kuelekea malishoni, labda kinjia ambapo kondoo walikuwa wanakimbia. Na mchungaji mzee anakwenda kule, ameshika fimbo iliyopindikana mkononi mwake, akipigapiga kando ya huo mkondo; labda amelemaa kidogo, mwenye umri wa miaka themanini; masharubu yakining'inia hadi kiunoni, labda, mwenye mvi kama kondoo aliokuwa akichunga. Naye aliona Kitu Fulani! Ee Mungu! Kilikuwa siri kwake.

159 Natumaini naweza kukuonyesha kitu usiku wa leo. Na tuna kidimbwi cha maji hapa, tayari.

160 Aliona kitu asichowahi kukiona hapo kabla. Naye alisema, "Yafaa nikichunguze Hicho." Kwa hiyo akageuka, na Neno la Mungu likamjia. Utukufu! Haleluya! Neno la Bwana likamjia.

Sasa, kabla hajapata kuondoka, ilimbidi atekeleze Neno la Bwana.

161 Na, kumbuka, Neno la Bwana siku zote hutenda maajabu. Akasema, "Nitajuaje kwamba Wewe u pamoja nami, kwamba amekutuma?"

Akasema, "Kuna nini mkononi mwako?"

Akasema, "Fimbo kavu."

162 "Itupe chini!" Amri ya kwanza Mungu aliyompa Musa. "Kama unataka kujua kwamba Mimi ni Mungu; una fimbo mkononi mwako, itupe chini."

Gideoni akasema, "Yako wapi maajabu ya Mungu?"

163 Akasema, "Weka mkate huo juu ya madhabahu, nitakuonyesha Mungu ni Nani." Na Yeye akaugusa kwa fimbo Yake; na moshi ukapanda juu, na ikateketezwa.

164 Musa akasema, "Nitasema ni Nani aliyenituma? Najuaje kwamba Wewe ni Mungu?"

165 Akasema, "Una nini mkononi mwako? Mimi ni Muumba wa uzima. Mimi ni Mungu atendaye maajabu." Na kabla ya Musa kuweza kuona Nguvu ya Mungu aliyetenda mambo haya yote, kwanza ilimbidi amtii Mungu. Akatupa fimbo chini, ikawa nyoka. Whiu! Loo, jamani! Nini? Ni . . .

Utii huja kwanza, kabla ya wewe kuona miujiza Yake!

166 Haya yaitwayo makanisa kote nchini leo, husema, "Vema, miujiza yote iko wapi? Tutatoa dola elfu moja kwa mtu ye yote atakayeruhusu, atakayefanya muujiza." Wewe, maskini, mwenye mashaka, uliyerudi nyuma, uliyekufa mara mbili, uliyeng'olewa kabisa!

167 Utaonaje muujiza, mpaka umekuwa mmoja? Utukufu! Muujiza wa neema ya Mungu, kumchukua mwenye mashaka asiyeamini na kumjaza na Roho Mtakatifu! Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, yeye hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu." Kama unataka kuona muujiza, fanyika mmoja. Mwache Mungu atende kazi ndani yako, kwanza. Sharti akukague, aweke lenzi mbalimbali machoni mwako, kwa sababu wewe ni kipofu, umekufa katika dhambi na makosa, kipofu kiroho, umekufa mara mbili. Hakika! Yambidi Mungu akupe Uzima, aguse macho yako ili uweze kuona; afanye muujiza, na kukufanya muujiza, na ndipo uweze kumuona Mungu atendaye maajabu. Hicho ndicho kitu cha kwanza.

168 Musa ilimbidi amwamini Yeye. Ilimbidi Musa atekeleze Hilo, kutenda ambalo Neno la Mungu limesema. Alitaka kuona kama huyo alikuwa Mungu au la. Yeye alisema, "Vema, musa, tenda ninalokuambia."

169 Sasa sikiliza hapa, usiku huu, ndugu, dada. Kama unataka kujua Mungu ni Nani, hebu tenda kile Yeye anachosema Hapa.

"Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, nawe utakuwa muujiza." Hiyo ni ahadi Yake. Hilo ndilo alilosema. Tekeleza Neno Lake, "Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu." Loo, hilo ni kwa mitume tu? "Na wao walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hapo ndipo palipoelekezwa ahadi.

170 Tekeleza Neno Lake, nawe utaona muujiza wa kweli. Kitu fulani kitatukia unapotekeleza Neno Lake. Kama Gideoni alivyotenda, alitenda ambalo Yeye alimwambia kutenda! Kama Nuhu alivyotenda, alitenda ambalo Yeye alimwambia kutenda! Kama Musa alivyotenda, alitenda ambalo Yeye alimwambia kutenda!

171 Kasema, "Tupa fimbo yako chini!" Kwa maneno mengine, "Ondoa kila kitu kilicho karibu nawe!" Amina. "Nipe Mimi!"

172 Unasema, "Nina hasira ya mkizi." Mpe Mungu, Yeye anajua jinsi ya kuituliza. "Nina tamaa baya sana." Yeye anajua jinsi ya kuiondoa. Unaona? Iweke tu mikononi Mwake, nawe utaona muujiza unavyoweza kufanya. Hilo ni kweli. Vema.

173 Musa ilimbidi ashughulikie Neno la Mungu, kabla, au, atii Neno la Mungu kabla ya yeye kuweza kuona maajabu ya Mungu. Lakini alipokwisha kuyaona, ndugu, hakuna kitu kitakachomzuia basi.

174 Ninamuona, kesho yake, na Sipora akiketi juu ya nyumbu huyu, na—na mtoto Gershomu kwenye kiweo cha babaye, au kiweo cha mamaye, hasa, masharubu yakining'inia chini namna *hiyo*. Ndugu, uso ule ulikuwa unatabasamu, macho hayo yanachezacheza kuelekea angani. Toka kwa mchungaji wa kondoo, hadi mtu mkuu wa Mungu; shujaa, akishuka kwenda kukomboa. Mwangalie Gideoni! Kulitukia nini? Ndiyo, bwana, akishuka kwenda na fimbo iliyopindikana, kuteka taifa. Aliliteka. Hakika aliliteka. Mungu alimwambia afanye hivyo.

175 Haidhuru jinsi inavyoonekana isiyo halisi, wewe fanya tu ambacho Mungu anakuambia kutenda. Utaona kwamba Neno Lake bado ni lile lile. Ondosha tu mawingu, Mwana bado anaangaza.

176 Yoshua, loo, yule mshindi mkuu! Loo, halifa wa Musa! Mtu ambaye Mungu alimpenda, shujaa hodari! Mtu ambaye Mungu alimpenda! Mungu alimwambia, "Kama nilivyokuwa na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe." Lakini kabla ya kuta kuanguka, Yoshua alipiga hatua taratibu sawa na amri za Kapteni Mkuu; kuuzunguka ule ukuta, mara kumi na tatu, kabla ya Nguvu za Mungu kupiga kitu hicho. Alitembea kuuzunguka ukuta, na akapiga tarumbeta, sawa na Neno la Mungu ambalo Kapteni Mkuu alimwambia huko alipokutana Naye. Alitembea kulingana na Neno la Mungu. Alifanya nini? Alitekeleza Neno, kabla ya kuuona huo muujiza.

177 Unajua, kupiga tarumbeta tu hakutikisi ukuta ukaanguka chini ambamo waweza kuendesha magari ya mashindano juu yake; huku unapiga tarumbeta. Lakini Mungu alisema, "Basi, tembeeni tu kuzunguka kuta, mara saba, na, siku ya mwisho, mara saba." Na mara kumi na tatu. "Na mnapouzunguka ukuta, mara ya mwisho, waacheni makuhani watangulie, pamoja na sanduku, kisha mpige tarumbeta. Na tarumbeta ikilia, kuta zitaanguka chini." Wangefanya nini? Aliona muujiza wa Mungu, baada ya kutekeleza Neno la Mungu.

Miujiza yako iko wapi? Tekeleza Neno Lake, kwanza.

178 Kuta zingewezaje kuanguka chini, na kuacha nyumba moja ndogo imesimama, nyumba ya kahaba? Kwa sababu alitekeleza Neno la Mungu. Kwa nini wengine wote walikufa, na kahaba akaishi? Alitekeleza Neno la Mungu, naye akaona muujiza wa Mungu. Hiyo ndiyo njia ya kuuona, kulitekeleza Neno.

179 Wale wana wa Kiebrania, kwenye ile tanuru ya moto. Walifanya nini kabla ya kuona muujiza wa Mungu? Walitekeleza Neno la Mungu. Walijua Yeye alikuwa ndiye Mungu. Wao walijua kuwa yeye ndiye Mungu aliyewapandisha kutoka Misri. Wao—wao walijua kwamba walikuwa . . . Yeye alikuwa ni Mungu yeye yule aliyekuwako siku zote, kwamba hapana budi Yeye alikuwa Mungu atendaye maajabu.

180 Naye alikuwa amewapa agizo "wasisujudu sanamu." Yeye habadiliki. "Kaeni na Neno Langu! Msizisujudie sanamu!"

181 Walisema nini? "Mungu wetu aweza kutuokoa na tanuru hii. La, sivyo, tutatekeleza Neno Lake!" Ndivyo ilivyokuwa. Kulitukia nini? Hapo wakaona muujiza wa Mungu, kwamba Mungu aliweza kuustahimili ule moto.

182 Kama wewe u mgonjwa? Tekeleza Neno Lake, uone kama Yeye huponya. Kama wewe u mwenye dhambi, na unataka kujazwa na Roho Mtakatifu; njoo, tubu, na ubatizwe katika Jina la Yesu Kristo. Na ukatekeleze Neno Lake, uone kitakachotendeka. Kama bado una ulimwengu ndani yako; na ninyi wanawake ambao bado mnakata nywele, bado mnajipaka vipodozi; ninyi wanaume ambao mngali mna hasira, na kugombana juu ya madhehebu yenu; Kama mkitaka kuona kama Yeye bado ni Mungu; litekelezeni na mkajilaze juu ya madhabahu Yake, muone kitakachotendeka. Yeye ni Mungu. Yawabidi mtekeleze Neno Lake, kwanza.

183 Danieli, kabla ya kuona muujiza wa Mungu, ungemtoa katika tundu la simba, kitu cha kwanza alichofanya ni kutekeleza Neno la Mungu.

184 Tangazo lilitolewa, "Kama mtu ye yote ataomba dua kwa Mungu mwingine ila sanamu hii, kwa siku *kadhaa*, atatupwa katika tundu la simba." Hakuna mtu angeweza kuomba kwa mungu mwingine isipokuwa yule Mfalme; ilibidi awe mungu, unaona, kwa siku thelathini.

185 Lakini Danieli alifanya nini? Alitekeleza Neno la Mungu. Sababu, Sulemani alipoiweka wakfu hekalu, aliomba, akasema, "Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida, po pote pale, na wataelekea kwenye hekalu hili takatifu, basi Wewe usikie kutoka Mbinguni." Hiyo ni kweli.

186 Daniel alitenda, kwanza. Tisho lilikuwa, "Utaingizwa katika tundu la simba." Lakini Danieli alitekeleza Neno la Mungu. Yeye alijua kwamba Mungu bado ni Mungu. Kama tu alivyofanya Gideoni; alijua kwamba Mungu, kama yeye yungali Mungu, basi maajabu Yake yako wapi? Na Danieli alijua alikuwa nabii, alijua alimpenda Mungu. Alijua alikuwa mtumishi Wake, na alijua Mungu aliweza kumwokoa na hao simba. Lakini kama alikuwa shidani, ametishwa, alielekeza uso wake hekaluni, na akaomba mara tatu kwa siku, vivyo hivyo kabisa. Alitekeleza Neno la Mungu, naye Mungu akamjaza sana Roho Mtakatifu hata simba hawakuweza kumla. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Alitekeleza Neno la Mungu kwanza.

187 Yona, katika tumbo la samaki, alitekeleza kwanza Neno la Mungu. Alijua alikuwa amekwisha, kuhusu mwili wake. Mikono yake ilifungwa, miguu yake ilifungwa. Mhubiri huyu kwa Mataifa alitupwa toka katika meli, akaingia katika tumbo la nyangumi, hata chini ya bahari. Sasa yuko katika hali gani! Lakini kwanza alijigeuza, mle ndani ya nyangumi huyo, mwani umezungushiwa shingoni mwake. Ambako, yule—yule nyangumi alikuwa akila mwani huu na kadhalika, kuweka vitamini katika mwili wake, vidonge vyake vya vitamini, na basi akampata mhubiri humo. Lakini mhubiri huyu akapata kujirudia! Haleluya!

188 Ee, ndugu, mhubiri, jirudie usiku huu! Toka kwenye hizo kanuni za imani za kale na kadhalika, umrudie Mungu aliye hai, Neno lililo hai.

189 Alijirudia, akageuka. Huwezi kumficha mtakatifu kutoka kwenye sala yake. Akageuka, na akaangalia, kila mahali ilikuwa tumbo la yule nyangumi, kumzunguka pande zote; mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini. Naye alitambua kwamba alikuwa katika tumbo la nyangumi, na chini kwenye kina cha chini cha bahari, na tufani baharini. Matumaini yote yaliondoka alipokuwa katika meli; na sasa alikuwa katika tumbo la nyangumi, mbali zaidi na tumaini kuliko alivyowahi kuwa. Na wakati alichoona tu ni tumbo la nyangumi, akasema, "Ni mambo ya ubatili na uongo. Sitayaamini tena. Lakini nitatazama kukabili hekalu Lako takatifu Bwana." Hekalu takatifu, hakuwa akiangalia chini; alisema, "Liko *kule* juu, kwa hiyo ninatazama kulikabili."

190 Ndipo basi akaona muujiza wa Mungu. Kwa namna fulani, oksijeni iliingia katika yule nyangumi. Alivuta hewa kama kawaida siku tatu, na akastarehe kidogo huku anasafiri, ili

apate kuchukua siku hizi arobaini . . . kuvuka, mji mwovu chini huko, kuhubiri Injili. Akapata kuburudika na oksijeni mpya kutoka Mbinguni. Isingeweza kutoka katika nyangumi yule, na isingeweza kutoka katika bahari, kwa hiyo ilibidi itoke kwa Mungu!

191 Ee, tupulizie usiku wa leo, Bwana, ile Oksijeni ya Neno la Mungu, katika Nguvu za kufufuka Kwake, tupate kuwa hai katika hii siku ya mwisho, siku ovu. Tupulizie, Ee Roho Mtakatifu! Ndiyo, ndugu. Puliza, Bwana, tujaze na Oksijeni!

192 Kama nilivyowaambia asubuhi hii kuhusu yule bata. Mara tu aliponusa harufu ya maji, hapakuwa na kitu cha kumzuia kwenda huko; milio yote ya kuku, na vitu vinginevyo vyote. Alikwenda moja kwa moja majini, kwa sababu alikuwa bata.

193 Sasa, kama kuna ye yote wenu mwenye asili ya bata, tuna dimbwi kubwa mno nyuma kule, unaona. Kama unaweza kunusa harufu, kama unafununu kwamba Mungu yuangali Mungu, kama unanusa harufu kutoka Mbinguni usiku wa leo, kwamba Mungu hutimiza Neno Lake na Yeye ni Mungu atendaye maajabu, na hujampokea Roho Mtakatifu bado; nusa harufu ya maji, kitu cha kwanza Yeye alichosema ufanye. Bila shaka. Tubu, toka kilindi cha moyo wako, na ujiweke mwenyewe kama kafara juu ya madhabahu; nawe utateketezwa, ya ulimwengu, na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho; na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, Yeye atakujaza na Roho Mtakatifu. Pitia njia ifaayo; si ati uje upeane mikono na mhubiri na kuandika jina lako katika kitabu, lakini, ufe kiasi kwamba huujui tena ulimwengu.

194 Habili alikufa kwenye madhabahu yale yale pamoja na mwana kondoo wake. Na njia pekee utawahi kupatana na Mungu, ni kufa kwenye madhabahu pamoja na Kristo, mpaka kila kitu kilicho karibu nawe kinakuwa cheusi. Fia hapo! Na uinukapo tena, utakuwa kiumbe kipya katika Kristo. Hakika.

195 Yona ilimbidi aamini Neno la Mungu, na kulitekeleza Hilo, kwanza. Sasa, labda alikuwa amelala kifudifudi, alipokwenda katika tumbo la nyangumi. Sababu wao walimtupa tu; akaenda mbio moja kwa moja ndani ya tumbo la nyangumi. Yule nyangumi akasema, "Vema, tutakwenda chini kwenye sehemu ya chini ya bahari sasa."

196 Na ninashangaa yule samaki aliwaza nini katika siku zile tatu, kitu cha ajabu kilikuwa kinatendeka. Sasa, unaona, maumbile, ya nyangumi, hayakutaka jambo hilo. Wala shirika la kanisa la kimadhebu halikulipenda. Lakini, loo, jinsi Yona alivyoipenda! Hakika, hasikii. Hakika aliipenda, kwa sababu ilikuwa hewa safi ambayo Mungu alikuwa anaipepea juu yake, naye akaishi. Mungu, tupepee Hewa safi!

197 Kama Yona aliweza kutenda muujiza kama ule, kwa kualiamini Neno la Mungu, kwa hekalu la kawaida; ambalo, mtu ambaye hatimaye alirudi nyuma, Sulemani, alijenga,

lakini akamwomba Mungu, katika maombi, kumbariki ye yote aliyeangalia kuelekea hakalu lile, na kuwatoa katika matatizo yao, po pote walipokuwa; na Yona aliweza kuamini, chini ya hali zile. Je! si twaweza kuamini zaidi sana, usiku wa leo, tukiangalia kuelekea Mbinguni; ambako, si mtu aliyerudi nyuma, si mtu aliyekufa na kudumu kaburini, kama Yona . . . au kama alivyokuwa Sulemani wakati huo, lakini Mungu aliye hai anayeketi mkono wa kuume wa Ukuu, Nguvu zote na mamlaka, na kuhubiri Neno na kumpeleka kwa Roho Mtakatifu kama shahidi jinsi alivyotenda. Amina. Amini Neno la Mungu, utaona miujiza ya Mungu. Lakini yakubidi Uliamini, kwanza. Hakika aliamini. Ndiyo.

198 Gideoni, baada ya kumuona Mgeni huyu akiketi chini ya mti, naye Gideoni kwa namna fulani alimuuliza maswali, kwanza. Alisema, "Kama Mungu bado yu Mungu, kama Mungu yu pamoja nasi, yako wapi matendo Yake ya ajabu?" Naye huyu—naye huyu Mgeni akiketi chini ya ule mti, alitenda nini? Yeye alipoigusa kafara ile kwa fimbo Yake ambayo Yeye alikuwa nayo mkononi Mwake, iliteketezwa. Naye akajua hilo lilikuwa tendo la Mungu, kwa hiyo akajua basi kwamba Mgeni yule chini ya mti, ambaye alionekana kama Mzee akiketi pale, alikuwa Neno lililofanyika mwili. Haleluya! Ilikuwa ni Neno lililo hai. Yeye alijua kwamba hilo lilikuwa Neno lililo hai, kwa sababu lilikuwa likitenda na kuishi katika wakati uliopo. Mungu atukuzwe, ndugu!

199 Upentekoste ni mzuri, lakini ni moto wa kuchorwa kama wewe mwenyewe hujampokea Yeye. Si wakati uliopita; wakati uliopo! Anafaa nini Mungu wa historia kama Yeye si Mungu yeye yule leo? Kama nilivyosema mara nyingi, itafaa nini kumpa kirumbizi wako, ndege, vitamini kufanya mbawa zake zikue, na kumweka katika kizimba na kumwacha humo? Kuna faida gani kufundisha kwamba kuna Mungu mwenye Nguvu, kisha kuwanyima watu haki ya kumtumikia Yeye? Amina. Hakika. Upuzi!

200 Kwa nini mna seminari hizi zote kila mahali, kama mtambo mkubwa wa kuatamia, unaoangua wahubiri? Unaona?

201 Sikuzote nimekisikitikia kifaranga cha mtambo wa kuatamia, kwa kweli hakuwa na mama ye yote. Hakujua kamwe alikotoka. Hana wa kumlea, alitokea tu kimitambo.

202 Hivyo ndivyo karibu alivyo mhubiri wa kiseminari ambaye anajua theolojia tu. Aweza awe na akili nyingi na ameadibishwa kama mwanachuoni ye yote awezavyo kuwa, angeweza kuhubiri katika lugha nyingi mbalimbali, lakini kama yeye hajui Mzazi wake ni nani!

203 Kama nilivyosema si muda mrefu uliopita; kama kuna kitu kijinga, ni nyumbu. Yeye hajui baba yake na mama yake ni nani. Ni kitu cha mchanganyiko, unaona, hajui yupi, baba gani,

mama. Hajui ni wa nani. Huyo ni kama baadhi ya Wakristo hawa wa mchanganyiko, kama wanavyojiita, wamezaliwa na madhehebu. Lakini farasi mzuri mwenye asili bora ana ukoo, anajua mambo yote.

204 Naye Mkristo aliye na asili bora anajua Ghala ya Mungu ilipo. Wao wanajua wamezaliwa kwa Neno. Neno linafanyika mwili ndani yao. Kila Neno asemalo Mungu, hawapingani Nalo; wao husema, "Ni kweli! Amina, na amina!" Huliitikia Hilo kwa "amina." kila wakati. "Amina! Amina!" Kitu fulani ndani yao huliitikia, Yeye Mwenyewe.

"Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele."

"Amina!"

Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

"Amina!"

205 "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa, ataokoka. Na ishara hizi zitafuatana na hao wanaoamini."

"Amina!"

206 Mzee kuku alisema, "Klak-klak-klak, na siku za miujiza zimepita."

Lakini, "Honk-honk-honk, nanusa harufu ya maji!"

207 Unaona, ndio hilo. Hilo ni sahihi. Unaona? Kwa nini? Unamjaribu Mungu. Unaona, ndivyo ilivyo, Mungu kwanza. Tekeleza Neno Lake, uone kama Hilo ni kweli. Hiyo ni kweli.

208 Yohana Mbatizaji alikuwa akiendelea barabara na kazi yake. Alipokuwa tu ki—kijana hatuna habari nyingi baba yake alikuwa mtu mzuri. Lakini hakumwamini Mungu. Mungu alikuwa ameyakinia kulileta kupitia kwa Elizabeti. Mtoto huyu kwa hiyo alimwambia, akamwambia ange—angechukua mimba ya mtoto huyu naye akalitilia shaka, ndipo akamfanya bubu.

209 Ningewazia moyo wa wazazi wa Yohana Mbatizaji, Elizabeti na Zakaria, walihuzunishwa kwa namna fulani, kwa sababu walijua wao ni wazee. Na mtoto huyu wa ahadi ambaye amezaliwa, ambaye Mungu amewatendea muujiza akamleta mtoto huyu ulimwenguni, walipokuwa wazee na wamepita umri. Walijua hilo, kisha mioyo yao ikahuzunika, kwa sababu hawakuweza kuishi muda mrefu kutosha kumwona akifanya kazi yake kubwa ya Mungu. Lakini walimweka wakfu kwa ajili ya jambo hilo! Mungu atukuzwe! Mahali fulani kupita nyota na mwezi, waliweza kuangalia chini na kuona jambo hilo. Hawatamuona kamwe mvulana huyu mdogo . . . Walikufa. Walikufa alipokuwa bado ni mtoto mdogo tu, kijana. Mvulana, aliondoka nyumbani mwake akaenda nyikani. Akalelewa huko, chini ya Uweza wa Mungu.

210 Mungu alimwambia, "Wewe u sauti ya mtu aliaye nyikani. Ninakupeleka. Nenda, ukapaze sauti!"

211 Jinsi ilivyombidi Yohana kungojea kila siku, huku akiwafukuza nyoka katika miamba, na kuyapiga teke mawe. "Loo, siwezi kungojea!"

"Unangojea nini, Yohana?"

212 "Hivi, nataka kusikia agizo Lake, hilo tu." "Ondokeni njiani, enyi nyoka!" Wangekimbilia kwenye miamba. Hiyo ndiyo sababu, hao Mafarisayo walipojitokeza, alisema, "Lo, enyi kizazi cha nyoka, kimbilieni kwenye miamba!"

213 Nasema jambo lile lile usiku wa leo. Enyi kizazi cha nyoka, kimbilieni kwenye maji! Amina. Mwajua ambalo nazungumzia. Kanda hizi, haya yananaswa kwenye kanda, yataenda ulimwenguni kote. Kimbilieni majini, kama mkitaka kuona matendo ya ajabu ya Mungu!

214 Yohana akifuatilia. Mtu fulani anayeonekana mzuri akaja; akasema, "Labda ni Yeye." Akaangalia. "La, huyo si Yeye. La. Mungu alinipa ahadi."

"Yohana, unasema Masihi yu hai leo?"

"Ndiyo."

"Yuko wapi?"

215 "Hapa duniani, mahali fulani. Sijui alipo Yeye, lakini nitamjua Yeye atakapokuja."

"Wajuaje?"

"Mungu aliniambia la kutazamia."

216 "Unajuaje utapona utakapoombewa?" Mungu aliniambia la kutazamia. "Unajuaje utampokea Roho Mtakatifu?" Nafuata Neno Lake. Yeye aliniambia la kutazamia, najua kinachofuatia, unaona. Unajua kinachofuatia? Kama utalitii Neno la Mungu, ahadi Yake itafuatia. Hawezi kudanganya; Yeye ni Mungu.

"Nini kinachofuatia?"

Yohana alisema, "Nitamwona wakati ajapo Yeye."

217 Wakasema, "Loo, hebu muangalie mtu huyu ajaye hapa. Huyo, amevikwa taji kichwani mwake, huyo hana budi kuwa ndiye Masihi, akiendesha farasi wale."

Akasema, "Huyo siye."

218 Akamwendea, akamwambia, "Si halali kwako wewe kumtwaa mke wa ndugu yako!" Walijua kulikuwa na kosa pale, sikia? Alimwendea, na kumwambia hilo. Ilikuwa Herode, unaona. Na, loo, ilimkasirisha mkewe sana, alimchukia maishani mwake mwote. Unaona?

219 Yohana alishikilia kutazama. Akasema, "Loo, nitamjua Yeye atakapokuja."

“Wajuaje?”

220 “Mungu aliniambia ningeona ishara, nayo ingekuwa ishara ya Masihi. Nitamjua Masihi kwa sababu ishara ya Masihi itakuwa pale.”

221 Mungu anajua kanisa Lake. Alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao.” Si “watakuwa Wamethodisti, Wabatisti, au Wapentekoste.” Lakini, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Huwajua waamini.

Wakati mwingine unasema, leo, “Wewe ni mwamini?”

222 “Loo, mimi ni Mmethodisti.” Vema, hilo huonyesha wewe si mwamini basi, unaona. “Mimi ni Mpentekoste.” Hilo pia laonyesha hu mwamini.

223 Ukiwa mwamini, unamwamini Mungu! Kila mtu anajua hilo, umekwisha tiwa muhuri na Ufalme wa Mungu; na muhuri upo pande zote mbili za ukurasa, ukija na pia ukienda. Unaona, waweza kuwajua. Sawa.

224 Alisema, “Nitamjua Yeye atakapokuja, kwa sababu kutakuwa na ishara. Nitaona ishara ya Masihi.” Siku moja aliangalia . . .

225 Loo, ndugu! Kwa nini? Alikuwa anaitazamia Hiyo, hivyo ndivyo alivyoitambua Hiyo. [Ndugu Branham anagonga kwenye mimbara—Mh.] Natumaini hilo litazama ndani. Wewe unaitazamia Hiyo? Unatazamia kitu fulani kutukia? Basi yajue Maandiko!

226 Sasa, makuhani hao wote wakisimama kila upande hapo, walikuwa wana akili mara tano ya Yohana. Hatuna habari ya alikoenda shuleni, siku moja. Bali makuhani walisimama hapo, kwamba babu za babu za babu zao walikuwa makuhani. Palisimama mtu pale ambaye alijua kila inchi ya lile gombo, manabii wote na Mwanzo, na yote yanayolihusu. Lakini, unaona, Yohana alikuwa anangojea ishara, Masihi! Alijua kama huyo alikuwa Mungu, pangetokea kitu fulani cha kimbinguni. Hilo ni kweli.

227 Hivyo ndivyo ilivyo leo! Kama wewe ni Mkristo, kuna kitu cha kimbinguni kilichokugusa. Kama hakikukugusa, umedanganyika. Ungali unaishi maisha yale yale uliyoishi kwanza, bado unapenda vitu vile vile ulivyovipenda hapo kwanza, bado ungali unavipenda, umedanganyika; hilo ni kweli, si mwana au binti wa Mungu.

228 Basi tunaona, Yohana alikuwa amesimama hapo siku moja, nao wanasema ni . . . nilisoma ha—ha—hadithi ndogo kumhusu Yeye, wakasema kwamba Yohana alikuwa upande mmoja wa mto, walikuwa wamemkataa upande ule mwingine. Hivyo ndivyo wanavyomfanya mtumishi wa Mungu, wanamkatalia katika kila madhehebu, kila shirika, kila kitu. Hakuwa na mimbara ambapo angesimama; lakini yeye amesimama katika

matope, yaliyomfikia magotini. Hakuwa na suti ya chakula cha jioni, huku ukosi wake umepinduliwa, pia. Hapana, bwana. Alikuwa amejifunga kipande cha ngozi ya kondoo mwilini, labda alionekana kama mshenzi akisimama pale.

229 Na hao makuhani wakasema, "Unataka kuniambia kwamba kuna wakati ambapo hekalu letu hili kuu, madhehebu yetu makuu, yataangamizwa?"

Akasema, "Hakika, yataangamizwa."

"Wajuaje hilo?"

230 "Unasomaje Andiko? Masihi yuaja, na Masihi huyo ataondoa sadaka ya kila siku. Danieli alisema hivyo! Nabii alisema hivyo!" Haleluya!

Loo, najisikia mwanadini zaidi wakati wote! (Sina budi kukoma.)

Wajuaje hilo? Nabii alisema hivyo!

231 Hivyo ndivyo Mikaya alivyojua kwamba hangeweza kumbariki Ahabu; Eliya alikwisha mlaani. Ni hayo tu. Ilimbidi akae na Neno. Ukitaka kuona kazi za Mungu, inakubidi ufuate Neno la Mungu. Alijua isingeweza kutokea.

232 Kwa hiyo kulitukia nini basi? Alitaka kuona kazi za Mungu. Yohana alisema, "Nitamjua atakapokuja."

233 Siku moja alikuwa amesimama pale, akasema, "Ndiyo, wakati unakuja ambapo sadaka ya kila siku itaondolewa. Masihi ndiye atakayekuwa Sadaka ya kila siku. Na chukizo la uharibifu litaanza."

"Rabi unatoa wapi hilo? Hilo ni kinyume cha kanuni ya imani yetu."

234 Lakini si kinyume cha Neno la Mungu. Huyo hapo nabii, kwa sababu Neno la Bwana lilikuwa na nabii. Hilo ni kweli.

235 Naye alisema kwamba, "Tazama, yule pale anasimama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Mtu wa kawaida, mdogo, mabega yameinama amesimama hapo, anashuka akaja kuelekea mtoni, akitembea pamoja na Lazaro. Mtu wa kawaida tu, amevaa kama watu wa kawaida; si kuhani, hana kilemba, hana taji, hakuna kitu; ni Kijana mwanamume maskini, Seramala, akashuka akaja, mikono Yake imejaa vibanzi, labda; aja anatembea akishuka.

"Unataka kuniambia . . . "

236 "Nini? Huwezi kumwona Yeye hapo? Tazama!" Humaanisha, tazameni kule juu, heshimu! Huyo hapo Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

237 Baadhi yao walisema, "Vema, unajua huyo ni Nani? Huyo ni yule mwana wa seremala. Sasa, tunajua kwamba jamaa huyo si nabii." Lakini, alikuwa hivyo. Alikuwa hivyo. Alijua. "Vipi? Hajui ambalo anazungumzia?" Ndiyo, alijua. "Angewezaje

kumtofautisha na mtu mwingine ye yote?" Masihi atakuwa tofauti. "Tutalijuaje?" Yohana aliona kitu wasichokiona wao.

238 Yategemea unatafuta nini. Usiku wa leo unaona nini? Unaona mtu mkubwa, anayejulikana sana, madhehebu makubwa, na kila kitu kinaangukia mapaja yako? Au, unaambatana na wachache wa Bwana waliodharauliwa? Unaiona Biblia? Unaona Neno la Mungu? Kama umezaliwa mara ya pili, utaliona. Hata utakapofanya hivyo, huwezi kuliona Hilo.

239 Huyu hapa anakuja. Akasema, "Yeye aliyeniambia, huko jangwani!" Loo, ndugu! "Yeye aliyeniambia 'paza sauti'! Nimekuwa nikipaza sauti hapa kwa miezi sita, tangu hapo mpaka kwenye miguu, na kila mahali hapa, juu na chini ya Yordani hii nikivuruga matope; nikigombana na ninyi wahubiri, wahubiri, nikiyakemea madhehebu yenu kila mahali, nikiwaudhi. Lakini Jambo lenyewe liko hapa, ninaliona!"

"Wewe unajuaje?"

240 "Mtu yule yule aliyeniambia 'kuwa sauti inayolia nyikani,' Mungu ameniinua mimi kwa kusudi hilo kasema, 'Yeye ambaye juu yake' mimi, 'nitamwona Roho."

241 Yohana alimjua Yeye. Alifanya nini? Alihubiri Neno kwanza, alitii lile Neno, naye aliona ishara ya Mungu. Na, kumbuka, haikuandikwa kwamba mtu mwingine ye yote aliyekuwa amesimama pale aliiona Hiyo. Yohana aliiona Hiyo peke yake. Inategemea unatafuta nini. Kwa nini? Yohana alikuwa anatii Neno. Makasisi na wengineo hawakuwa wanatii Neno. Yohana alikuwa anatii Neno, agizo lake, na aliliona Hilo. (Tutaharakisha upesi; yatubidi.)

242 Martha, kaburini. Alikutana na Neno la Mungu. Aliliamini. Kabla ya kuona muujiza wa Mungu, ilimbidi aamini Neno la Mungu na kulitekeleza. Alisema, "Bwana, kama ungalikuwepo hapa, ndugu yangu asingalikufa."

243 Akasema, "Martha, Mimi ndiye huo ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, lakini ataishi. Naye kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe. Je! Unayasadiki hayo?"

Akasema, "Ndiyo, Bwana." Unaona, kutekeleza! "Ninaamini."

"Unaamini nini, Martha?"

"Kwamba Wewe u Kristo yule ajaye ulimwenguni."

Akasema, "Mmemzika wapi?"

244 Akashuka chini kule kaburini, na Huyo hapo amesimama hapo. (Akasema, "Nataka kuona kama kweli ananiamini kweli kwamba Mimi ni Neno.") Akasema, "Liondoeni jiwe."

245 Akaenda kutekeleza Neno! Ilimbidi kufanya hivyo, apate kuona kifo kinageuzwa kuwa uzima.

246 Na njia pekee utaweza kuona kifo kikigeuzwa kuwa uzima, ni kuchukua Neno Lake na kulitekeleza!

247 Kama wewe u mwenye dhambi, chukua Neno Lake ukalitekeleze, ndipo utaona muujiza wa Mungu. Unakuwa muujiza wa Mungu.

248 Kama wewe u mgonjwa, chukua Neno la Mungu! Daktari anasema, "Utakufa." Chukua Neno la Mungu ukalitekeleze, hilo litaleta uzima mpya. Loo, jamani!

249 Samahani kwa kuwaweka muda mrefu sana. Yamebaki machache tu, kisha nitaondoka. Unaona, yamesalia machache. Kweli, nitaondoka. Ninasikitika kuchukua wakati wa ndugu yangu. Waona, linawaachia masaa mawili tu kwa ajili ya jambo hilo. Angalia.

250 Yule mwanamke pale kisimani. Yeye alikuwa mwenye dhambi. Alikuwa na waume watano. Akaja pale siku moja, kuchota maji. Alianza kuchota maji, naye akasikia Mwanamume akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

251 Akatazama huku na huko, akasema, "Si kawaida kwa Wayahudi kuzungumza na Wasamaria. Mimi ni mwanamke wa Samaria. Na si kawaida. Kwa nini Wewe uzungumze nami?"

252 Yeye akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani ambaye unazungumza naye, ungaliniomba Mimi maji."

253 "Mbona," akasema, "kisima ni kirefu, na Wewe huna kitu cha kutekea." Akasema, "Je, je—je utatekaje maji?"

254 Naye akasema, "Maji nitakayokupa yatakuwa chemchemi ya Maji, chemchemi, inayobubujikia nafsini."

255 Akasema, "Sasa, ngoja kidogo. Wewe u Myahudi, unaabudia Yerusalemu, na baba zetu waliabudu katika mlima huu," na kadhalika.

256 Akasema, "Niamini Mimi! Saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo hamtaabudia Yerusalemu wala katika mlima huu. Lakini Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho."

257 Bila shaka maskini mwanamke yule alisema, "Sasa, ngoja kidogo. Jamaa huyu ni nani hata hivyo?" Alitaka ajue Yeye alikuwa Nani, kwa sababu ilibidi amjulishe kwa Wasamaria. "Yeye ni Nani?" akasema.

258 Alizungumza naye dakika chache. Akasema, "Mwanamke, nenda kamlete mumeo, uje naye hapa."

259 (Lakini akasema, "Sasa ameanza ujanja," unaona.) Akasema, "Sina mume ye yote." Aha-loo!

260 Ndipo fimbo ikaigusa ile kafara. Unaona, jambo fulani lilitukia. Kulitukia nini? Aliona muujiza wa Mungu. Akasema, "Umesema ukweli. Kwa sababu, umekuwa nao watano, naye uliye naye sasa siye mume wako, hapo umesema kweli."

261 Akageuka. Alijua kwamba Mungu huyo, kwa wale watu, amekufa kwa miaka kadha; makuhani wao na marabi wao, na kadhalika, walikuwa wamezungumza kuhusu Mungu. Lakini ilikuwa imeahidiwa katika Biblia kwamba Mmoja anakuja!

262 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa U nabii." Unaona? "Twajua ya kwamba yuaja Masihi." ("Sasa hebu niwe na hakika ya hili.") "Twajua ya kuwa yuaja Masihi." ("Nitamuuliza Yeye hili, na nitaona neno Lake ni nini; mtu hawezi kuniambia hilo, yeye ambaye hamjui Mungu.") "Twajua ya kuwa yuaja Masihi, aitwaye Kristo. Na, Yeye ajapo, hili ndilo jambo ambalo atafanya atakapokuja Yeye. Tunamtazamia."

Akasema, "Mimi Ndiye."

263 Hilo lilitosha. Hilo lilitosha. Akakimbia mjini. Akasema, "Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo yote niliyotenda."

264 Kabla ya kuweza kuleta ujumbe ule, ilibidi kwanza aone muujiza wa Mungu. Kabla ya kuweza kuona muujiza wa Mungu, ilimbidi kuliamini Neno la Mungu. Hiyo ni kweli kabisa.

Loo, jamani, jinsi tungeweza kuelendelea! Hebu tumchukue mwingine.

265 Pentekoste. Baada ya kutembea na Neno, baada ya kuliona Neno, baada ya kuamini Neno, lakini kabla ya kuona mwujiza wa Pentekoste, iliwabidi walitii Neno. Unaona? "Nendeni kwenye mji wa Yerusalemu," Neno likasema, "mkangoje hapo mpaka mvikwe Uwezo utokao Juu."

266 Sasa, vipi kama siku nane zilipita, Mathayo akaangalia upande wa Marko, akasema, "Wajua nini? Nimehisi kitu cha ajabu hivi majuzi, hicho lazima kilikuwa Roho Mtakatiu. Alituambia kungojea hapa. Unaona, hicho hakina budi kuwa Ndiye."

"Loo, hebu na tungojee siku nyingine."

267 Siku ya tisa yaja. "Vyema, sasa, Yeye alituambia tukwee hapa, siku tisa zilizopita. Hakika, hamuamini tumempokea? Naamini tulimpata tulipomwamini Yeye. Na wewe je?" Loo, enyi Wabaptisti wazuri! Mnaona? Akasema, "Ninaamini. Ninaamini tumempata, kwa sababu Yeye alituambia tukwee huku. Na unajua ninaloamini? Ninaamini, mara tu tulipofika hapa, tulitii alilonena Yeye:"

268 Lakini alisema nini Yeye? Yeye hakusema, "Mtakapofika juu kule, mtampata." Hakusema, "Ngojeeni siku tano, au siku tisa." Alisema, "Mpaka!" Ndilo hilo. "Wao wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya." Unaona?

269 Unafanya nini? Chukua Neno Lake, litekeleze Hilo na ukae Nalo. Kila siku, simama kidole kwa kidole na Shetani, ukiwa Nalo, "Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa!" Haina budi kutimia!

Unatekeleza Neno, unaona, ndipo utaona muujiza wa Mungu. Hiyo ni kweli. Lakini kwanza yakubidi ulitekeleze.

270 Walikwea kule nao wakalitii Neno, wakakaa huko.

271 Siku ya tisa ikaja. Naweza kumsikia Petro akisema, "Mnajua, ninyi ndugu mnafikiriaje?"

272 Penginepo Marko aliinuka, na kusema, "Je! mwajua? Ndugu zanguni, hebu na tulikubali kwa imani, kwa sababu tunatii." La, hamtii kikamilifu.

273 Ulisema, "Nilikuwa nimebatizwa katika jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Hilo, huko siyo kutii kikamilifu. Unaona? Unasema, "Nilijiunga na kanisa." Huko si kutii, unaona. "Ninakariri Imani ya Mitume." Huko bado si kutii. "Loo, ndugu, nimeacha kusema kwangu uongo na kuiba. Sitendi tendo lo lote baya." Huko bado si kutii.

274 Sharti iwe Uzao! Sharti kutukie kitu. Huna budi kufa, na Kitu fulani kizaliwe ndani yako.

275 Loo, baada ya kungojea siku nyingi sana, siku tisa zilipita. Walisema, "Hebu na tumkubali tu, na tuendelee na huduma yetu. Ulimwengu unakufa kule nje, kwa nini tuendelee kungojea?"

276 Naweza kumsikia Petro akisema, "Lakini, mnajua, Kitu fulani kinaniambia hilo si sahihi bado. Huko siyo kutii sawasawa kabisa Neno. Unaona, kama tunatazamia kuona mwujiza ambao Mungu alituahidi, wa kutupelekea ahadi ya Baba, yatubidi tungojee hapa mpaka kitu kitukie. Kwa sababu, Maandiko yalisema kwamba ingetokea katika namna hii, Yoeli alisema, 'Nitawamwagia watu wote Roho Yangu. Wana wenu na binti zenu watatabiri. Nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho Yangu. Nitatoa ishara na maajabu katika Mbingu na katika nchi.' Nabii Isaya alisema, 'Na kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitanena na watu hawa, na hii ndiyo siku ya sabato ambayo wanapaswa kuingia. Kwa yote haya, wasingesikia hilo.' Sasa, ndugu zanguni, tusingeweza kutembea kutoka hapa namna hiyo, bila hata ya kuona tukio lo lote kabisa, unaona. Yabidi tupate kitu fulani, kwa sababu Yeye alisema, 'Ngojeni hapa mpaka mpate Uwezo.' Sasa, sijawa na Nguvu zaidi ya vile nilivyokuwa nilipokuja humu ndani. Nimeshinda hapa usiku kucha, nimeshinda hapa usiku uliopita, nimeshinda hapa siku tisa. Niko vile vile tu hapa nilivyokuwa nilipokuja humu ndani. Alituambia tutapokea Uwezo, kwa hiyo na tuendelee kungojea."

277 Kisha, mara, walipotii kabisa Neno la Mungu, basi wakaona mwujiza wa Pentekoste. Waliona Moto ukianguka humo jengoni. Nguzo ile ya Moto ikashuka, miongoni mwa watu; na miali mikubwa, kama ndimi za moto, zikakaa juu ya kila mmoja wao. Nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.

278 Kitu kilitukia lini? Wao walipo—walipofanya uamuzi wao kwamba, kwamba tayari wamekwisha mpokea? La. Walipotii kikamilifu Neno la Mungu, waliona muujiza wa Pentekoste. Hivyo ndivyo ilivyo leo, yakubidi ufanye jambo lile lile.

279 Sasa, marafiki, nitamalizia hasa katika hili. Sitapindua ukurasa mwingine. Vema, mtu anayefuata awe tayari nitakaponena hili.

280 Sasa, ingawa aliitwa kila kitu kiwezacho kuitwa, kibaya, "mtakatifu anayejifiringisha, mpentekoste, mvunja kanisa, mnafiki, Beelzebuli, mwota ndoto." Kila kitu kiwezacho kuitwa, tunaitwa. Lakini wanafanya nini, wanakuita nini? "Mwota Ndoto, Beezebuli, nabii wa uongo, Yesu Tu," kila kitu kiwezacho kuitwa, kila kitu kibaya kiwezacho kuitwa.

281 Lakini, kwa kuamini Neno la kweli la Mungu, nabii Wake wa kweli wa Neno, tunafanya nini? Tunaona mambo tunayoona.

Loo, watakuja toka Mashariki na Magharibi,
Watakuja kutoka nchi za mbali,
Kula na Mfalme wetu, kula kama mgeni Wake;
Jinsi walivyobarikiwa hawa wasafiri!
Wakiangalia, uso Wake mtakatifu
Ukiwaka kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Watang'ara kama johari katika taji Yake.

Yesu yuaja hivi karibuni,
Majaribu yetu yataisha
Loo, je kama Bwana wetu angekuja wakati huu
Kwa wale walio huru na dhambi?
Loo, basi ingekuletea furaha,
Au huzuni na kukata tamaa kabisa?
Wakati Bwana wetu atakapokuja katika utukufu,
Tutamlaki hewani.

282 Kwa nini? Tunatekeleza Neno Lake! Amina. Itana cho chote unachotaka. Tunaona ishara ya Masihi katikati yetu. Tunaona Nguzo ya Moto. Haiwezi kukanushwa! Watuite cho chote wanachotaka kutuita. Mungu yupo hapa. Sayansi imeipiga picha. Kwa nini? Kutii Neno Lake! Haijawahi kufanyika katika historia, lakini hata hivyo jicho la kimashine la kamera linasema ni Yeye, kuna Nuru iliyoigusa lenzi. Kwa nini? Kuchukua Neno la Mungu kwanza! Acha madhehebu yakufukuze, yakitaka. Acha wote wakupe kisogo, ukitaka. Lakini tekeleza Neno la Mungu, kama ukitaka kuona maajabu ya Mungu!

283 Yesu aliahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

284 Malaika yule alishuka, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa binadamu, akaelekeza mgongo Wake kwenye hema, na akamwambia . . . huku hajui Ibrahimu alikuwa nani, akijifanya,

kasema, "Ibrahimu." Siyo Abramu; Yeye alikuwa tu amebadili jina lake hivi punde, siku chache hapo awali. "Yu wapi mkeo Sara?" Siyo S-a-r-a-i. S-a-r-a! "Yu wapi Sara mkeo?" Kamwita kwa jina lake la kibaba, naye mkewe kwa jina lake la binti mfalme. Loo! Yeye alikuwa nani? Ibrahimu alijua papo hapo huyo alikuwa Nani.

Akasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

285 Akasema, "Nitakurudia, Ibrahimu. Mimi, nitakurudia, sawa na ahadi Yangu ambayo nilikupa, kwa sababu umengojea sasa miaka hii yote. Umeingojea miaka ishirini na mitano. Ulishikilia Neno, ukilitekeleza Neno. Ulikataa hata kwamba wewe ni wa ulimwengu huu. Umekuwa msafiri na mgeni. Unautafuta Mji ujao, Ambao Mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu. Nilikuahidi kwamba, kupitia kwa mtoto huyu atakayezaliwa, kwamba yeye . . . ungekuwa baba wa mataifa mengi. Nimeahidi hilo. Umelitekeleza hilo Neno, sasa utaona muujiza wa Mungu."

"Nitalionaje, Bwana wangu?"

"Yu wapi mkeo, Sara?"

"Hemani, nyuma Yako."

Kasema, "Nitakurudia, sawa na wakati uu huu mwakani."

286 Naye Sara akacheka moyoni mwake, akasema, "Yawezekanaje mimi, mwanamke mkongwe; na bwana wangu, mzee, pia; kuwa na furaha tena?"

Akasema, "Mbona Sara amecheka?"

287 Alikuwa ametekeleza Neno la Mungu. Alikuwa anaona muujiza wa Mungu.

288 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Unaona, tekeleza Neno la Mungu, nawe utaona mwujiza wa Mungu.

289 Ilikuwa ni nini? Tuliposimama hapa, si muda mrefu uliopita, tukihubiri *Nyakati za Kanisa*, na kuzielezea, na ishara ile ndogo iliyopo pale, tukazichora hapa kwenye ubao. Na papa hapa, katika kusanyiko hili, mbele ya watu wengi kuliko wanaoketi hapa sasa, mara tu nilipomaliza kuzungumza, Nuru ilishuka ikimetameta, na ikaenda nyuma kule na kuning'inia kwenye ukuta ule. Na kivuli kikaja juu yake, huku kila mtu anaiangalia, na ikazipima hizo nyakati za kanisa sawa kabisa na vile zilivyo pale. Ni wangapi wapo hapa sasa ambao walikuwa hapa siku ile, inueni mikono yenu. Unaona? Mkiiaangalia na macho yenu wenyewe! Ilikuwa nini? Kwanza, kuamini Neno la Mungu, kuhubiri Neno la Mungu, kulipokea Neno la Mungu; nasi tukaona muujiza wa Mungu akihakikisha Neno, kwamba lilikuwa kweli.

Loo, Yesu yuaja hivi karibuni, (wote pamoja)
Majaribu yetu basi yataisha.
Loo, je! kama Bwana wetu wakati huu angekuja
Kwa wale ambao ni huru na dhambi?
Loo, basi ingekuletea furaha,
Au huzuni na kukata tamaa kabisa?
Bwana wetu ajapo katika utukufu,
Tutamlaki hewani. Amina

290 Kwa nini? Tunaamini Neno Lake, tukiweka Mafuta katika taa, itengenezwe na kuwaka, "Nuru yenu na iangaze hata watu wengine wapate kuyaona matendo yenu mema, matunda yenu, wamtukuze Baba yenu aliye Mbinguni." Na nini kitatukia? Kuamini Neno la Mungu, na kutekeleza Neno la Mungu, tutakutana naye hewani. Hapana shaka kamwe. Mungu awabariki.

291 Nitamalizia, nimefikia kama theluthi moja. Nitalimalizia wakati mwingine, Bwana akipenda. "Kama Bwana yu pamoja nasi, basi yako wapi matendo Yake ya ajabu?" Unaona? Unaliamini?

292 Ee Mungu, tujalie kuona mwa—mwaka ujao. Tujalie kuuona mwaka ujao, mpaka mioyo yetu haitaridhika na madhehebu ya kanisa, au kanuni ya imani, na kupeana mikono, au hii, iitwayo dini. Jalia tusiridhike hata tutakaposikia Nguvu itendayo maajabu katika Mungu ikiutoa, katika mioyo yetu binafsi, kuutoa ulimwengu, na kumuumba Kristo. Sasa, si eti usiku wa leo, na kesho uanze kufanya kitu kingine; lakini tukue katika Yeye, kufikia kimo Chake. Tukue kama Yeye, hata tutakapomlaki. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi katika Chemchemi kwa ajili yako;
Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi katika Chemchemi kwa ajili yangu.

293 Baba yetu wa Mbinguni, kwa unyenyekevu wa nafsi na roho, nimepwewa sauti, na maneno haya machache yaliyokatika au yaliyovunjika-vunjika, Bwana, naomba kwamba Wewe utayachukua na kuyaunganisha pamoja; kwa kuwa sijui jinsi ya kutenda jambo hilo, lakini ni kutamka tu kinachokuja bongoni mwangu. Liweke chini katika moyo wa kila mtu, nao na walione na kuliamini, kwa hali ambayo imetolewa. Na, Baba, itawafanya wafikiri, itamleta Kristo kwao. Tubariki usiku huu, Baba. Twangojea, tukilitekeleza Neno la Mungu.

294 Wabariki ndugu hawa, Bwana. Nisamehe mimi, Baba, kwa kuchukua sehemu fulani ya wakati wao. Naomba kwamba Wewe utawapa upako wa Roho Mtakatifu, hata kwamba Nguvu ya Mungu itaanguka katika jengo hili hapa, na wenye dhambi

watakuja madhabahuni na—na kulia wakielekea Kalvari, na kwamba wagonjwa wataponywa, na ishara kubwa na maajabu yatafanyika, nasi tutaona Nguvu itendayo miujiza ya Mungu aliye hai. Twangojea hilo, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

295 Bwana asifiwe! Mnampenda? Kama Mungu yu pamoja nasi, hebu na tuone ishara Yake!

296 Ishara ya Masihi iko wapi ambayo ni ile ile jana, leo, na hata milele? Kama Masihi ni yeye yule, atakuwa na ishara ile ile. Yuko wapi? Ni wa madhedhebu gani? Tutajiunga na madhehebu yapi, na kumuona Masihi, ishara Yake? Twaweza kuingia nyumba ipi, kuiona? Lifikirieni jambo hilo.

Samahani, Ndugu Neville.

*Kama Mungu Yu Pamoja Nasi, Basi Yako Wapi Matendo Yake Ya Ajabu?* SWA61-1231E
(If God Be With Us, Then Where Is All The Miracles?)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Decemba 31, 1961, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org